JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MASWALI YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI MWAKA 2021

## MAARIFA YA JAMII & STADI ZA KAZI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI (PSLE) 2021

# MAARIFA YA JAMII NA STADI ZA KAZI

*Kimechapwa na:*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S. L. P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© **Baraza la Mitihani la Tanzania, 2021**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

DIBAJI ........................................................................................................ iv
1.0 UTANGULIZI ........................................................................................ 1
2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA KILA SWALI 2
2.1 Sehemu A: Maswali ya Kuchagua Jibu Sahihi ................................ 2
2.2 Sehemu B: Maswali ya Majibu Mafupi........................................... 53
3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA KILA UMAHIRI ........................................................................................... ..61
4.0 HITIMISHO ........................................................................................ 61
5.0 MAPENDEKEZO ................................................................................ 62
Kiambatisho.............................................................................................. 64

# DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa Taarifa ya Uchambuzi wa Majibu ya maswali ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi mwaka 2021 kwa somo la Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi. Taarifa hii ina lengo la kutoa mrejesho kwa watahiniwa, walimu, watunga sera, watunga mitaala na wadau wengine wa elimu. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mitihani ni kiashiria kimojawapo kinachoonesha ujuzi na maarifa ambayo watahiniwa waliweza kupata, au kutopata katika somo la Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi.

Katika taarifa hii, uchambuzi wa kila swali umefanyika. Changamoto mbalimbali walizozionesha watahiniwa wakati wa kujibu maswali zimeainishwa pia. Aidha, uchambuzi wa kiwango cha ufaulu kwa kila umahiri kimeanishwa ili kuweza kubaini ni umahiri upi ulikuwa na changamoto zaidi miongoni mwa watahiniwa.

Vilevile uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa waliopata alama za juu walikuwa na maarifa yaliyowawezesha kubaini matakwa ya maswali, wakati watahiniwa wenye uelewa mdogo hawakuweza kubaini matakwa ya maswali. Kwa ujumla watahiniwa wengi waliofanya vibaya walitoa majibu yasiyo sahihi. Wengine hawakujibu baadhi ya maswali au walijibu jibu zaidi ya moja kwa swali la 1 – 40, kinyume na maelekezo ya mtihani.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa mrejesho huu utawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Ni matumaini ya Baraza la Mitihani kuwa mamlaka husika zitahakikisha kuwa changamoto zilizoainishwa katika taarifa hii zinapatiwa ufumbuzi ili kuongeza maarifa na ujuzi kwa watahiniwa wa mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi.

Mwisho, Baraza la Mitihani linapenda kutoa shukrani za dhati kwa maafisa mitihani na wengine wote waliohusika katika kuandaa taarifa hii.

Dkt. Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) wa somo la Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi ulifanyika tarehe 8 Septemba, 2021. Jumla ya watahiniwa 1,132,084 walisajiliwa kufanya mtihani huu ambapo watahiniwa 1,107,778 sawa na asilimia 97.9 walifanya mtihani. Jumla ya watahiniwa 788,528 sawa na asilimia 71.2 walifaulu mtihani katika somo hilo.

Somo la Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi lilikuwa na jumla ya maswali 45 yaliyogawanyika katika sehemu kuu mbili; A na B. Sehemu A ilikuwa na maswali 40 ya kuchagua na sehemu B ilikuwa na maswali 5 ya majibu mafupi.

Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote kutoka katika sehemu zote mbili. Aidha, katika swali 1 – 40 watahiniwa walipewa machaguo matano katika kila swali ambayo kati yake kulikuwa na jibu sahihi. Watahiniwa walielekezwa kuchagua jibu sahihi na kisha kuweka kivuli katika herufi ya jibu sahihi katika fomu maalum ya kujibia (OMR). Katika kujibu swali la 41 – 45, watahiniwa walielekezwa kuandika majibu yao katika nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia kalamu ya wino wa bluu au mweusi, upande wa nyuma wa karatasi ya OMR.

Katika taarifa hii, herufi ya jibu sahihi imewekwa alama ya (*) katika majedwali na chati. Zaidi ya hayo, asilimia ya watahiniwa ambao hawakufuata maelekezo ya namna ya kujibu swali imewekwa katika uchambuzi na kupewa jina “Mengine”. Hii inamaanisha watahiniwa hao hawakujibu kabisa swali husika, au walichagua jibu zaidi ya moja kama inavyoonekana katika majedwali na chati. Katika uchambuzi huu, idadi ya watahiniwa na asilimia yao katika kila chaguo imeoneshwa. Ubora wa kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika kila swali unategemea idadi ya watahiniwa waliochagua jibu sahihi. Katika uchambuzi huu pia, sababu za watahiniwa kuchagua jibu, kuandika jibu sahihi au vipotoshi zimeainishwa.

Kigezo cha ukokotoaji wa kiwango cha ufaulu kinategemea idadi ya watahiniwa waliochagua au kuandika jibu sahihi kama ifuatavyo: endapo watahiniwa asilimia 0 hadi 39 watakuwa wamechagua au

kuandika jibu sahihi, ufaulu katika swali utaelezwa kuwa ni hafifu. Endapo watahiniwa kati ya asilimia 40 hadi 59 watakuwa wamechagua au kuandika jibu sahihi, ufaulu katika swali hilo utaelezwa kuwa ni wa wastani. Aidha, ufaulu katika swali utaelezwa kuwa mzuri endapo watahiniwa asilimia 60 au zaidi watakuwa wamechagua au kuandika jibu sahihi.

Umahiri uliotahiniwa katika PSLE 2021 somo la Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi ni *Kutambua matukio yanayotokea katika mazingira yanayomzunguka* swali la 1-3, 5-11, 41 na 43; *Kutambua misingi ya uzalendo katika jamii* swali la 12-23 na 42*; Kutumia ramani na elimu ya anga katika maisha ya kila siku* swali la 24-28 na 45*; Kufuata kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishaji mali* swali la 4, 6, 29-35 na 44. Vilevile *Kutumia misingi ya unadhifu swali la* 39 na 40, *Kumudu mapishi mbalimbali,* swali la 38; *Kusanifu kazi za sanaa* swali la 36 na *Kutumia stadi za ujasiriamali* swali la 37*.*

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA KILA SWALI

### 2.1 Sehemu A: Maswali ya Kuchagua Jibu Sahihi

**Swali la 1:** Maji ni muhimu kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini Tanzania. Bainisha vyanzo vikuu vitatu vya rasilimali hiyo.

A Mvua, maziwa na bahari
B Bahari, visima na mito
C Mvua, maji yaliyo juu na chini ya ardhi
D Maziwa, mito na chemchemi
E Visima, chemchemi na mvua

**Jedwali Na. 1: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 395,910 | 204,855 | 111,272 | 225,521 | 155,682 | 14,559 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 35.7 | 18.5 | 10.0 | 20.4 | 14.1 | 1.3 |

Swali lilimtaka mtahiniwa kutambua vyanzo vikuu vitatu vya maji. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa hafifu kwani ni watahiniwa 111,272 (10.0%) tu walichagua jibu sahihi *C, Mvua, maji yaliyo juu na chini ya ardhi.* Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu vyanzo vya maji. Walielewa kuwa tunapata maji kutoka juu wakati mvua inanyesha. Pia, walitambua kuwa tunapata maji kutoka kwenye maeneo mbalimbali ya maji yaliyopo kwenye uso wa dunia. Watahiniwa hao pia walikuwa na uelewa wa vyanzo vya maji vya ardhini.

Watahiniwa 395,910 (35.7%) walichagua kipotoshi *A, Mvua, maziwa na bahari.* Kipotoshi hiki kilichaguliwa na watahiniwa walio wengi kutokana na ukweli kuwa mvua ni chanzo cha maji kinachopatikana katika maeneo mengi nchini. Uwepo wa maziwa makuu hapa nchini, na hasa uwepo wa ziwa Victoria ambalo kwa hivi karibuni maji yake yamesambazwa katika mikoa mbalimbali kumewafanya watahiniwa wengi kuamini kuwa ni chanzo kikuu cha maji. Pia uwepo wa Bahari ya Hindi ambayo hutumika kwa shughuli za uvuvi na usafirishaji ambazo ni shughuli za kiuchumi hapa nchini, kumewafanya watahiniwa kuchagua kipotoshi hiki. Hivyo, watahiniwa hawakuweza kutambua kuwa maziwa na bahari ni chanzo kimoja cha maji ambacho ni maji yaliyo juu ya ardhi. Kwa hiyo, katika chaguo hilo kuna aina mbili tu za vyanzo vya maji ambavyo ni mvua na maji yaliyo juu ya ardhi.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 204,855 (18.5%) walichagua kipotoshi *B, Bahari, visima na mito.* Uchaguzi wa kipotoshi hiki ulitokana na uzoefu walionao juu ya vyanzo vya maji vitumiwavyo katika mazingira wanayoishi. Hii inaonesha kuwa walishindwa kung’amua kuwa vyanzo vilivyotajwa katika kipotoshi B ni viwili tu.

Vyanzo hivyo ni maji yaliyo juu (bahari na mito) na chini ya ardhi (visima), ambapo mvua kama chanzo kikuu cha maji hakikutajwa.

Kipotoshi *D, Maziwa, mito na chemchemi* kiliwavutia watahiniwa 225,521 (20.4%). Watahiniwa hao hawakubaini kuwa chaguo hili limetaja vyanzo viwili tu vya maji; maziwa na mito ambayo ni maji yaliyo juu ya ardhi na chemchemi ambayo hutokana na maji ya chini ya ardhi.

Vile vile watahiniwa 155,682 (14.1%) waliochagua kipotoshi *E, Visima, chemchemi na mvua* hawakuelewa kuwa visima na chemchemi ni chanzo cha maji yaliyo chini ya ardhi. Hii inafanya kipotoshi hiki kuwa na vyanzo viwili tu vya maji ambavyo ni mvua na maji yaliyo chini ya ardhi. Watahiniwa 14,559 (1.3%) hawakujibu swali hili au walitoa jibu zaidi ya moja.

**Swali la 2:** Kupungua kwa theluji katika mlima Kilimanjaro kumesababishwa na ongezeko la joto katika uso wa dunia. Ni shughuli ipi inaweza kutumika kukabiliana na tatizo hilo?


A Kuchoma misitu na kukata miti
B Kulima kandokando ya milima
C Kupanda miti na kutunza mazingira
D Uvunaji ovyo wa misitu
E Kufuga mifugo mingi katika eneo dogo

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubaini shughuli inayoweza kutumika katika kukabiliana na upungufu wa theluji katika mlima Kilimanjaro. Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwani watahiniwa 729,828 (65.9%) walichagua jibu sahihi *C, Kupanda miti na kutunza mazingira*. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu faida za kupanda miti. Walitambua kuwa kupanda miti huzuia mmomonyoko wa udongo, husababisha kutokea kwa mvua na hutunza vyanzo vya maji. Haya ni mambo ambayo huboresha mazingira na matokeo yake ni uwepo wa joto la wastani, au kupungua kwa joto na hivyo kuzuia kuyeyuka kwa theluji.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 203,226 (18.3%) walichagua kipotoshi *A, Kuchoma misitu na kukata miti.* Uchaguzi wa jibu hili lisilo sahihi unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakutambua vyanzo vya uharibifu mazingira. Uchomaji misitu husababisha kupungua kwa mvua na kutokea kwa ukame. Watahiniwa waliochagua kipotoshi hiki hawakutambua kuwa jambo hili husababisha kupungua kwa theluji ya Mlima Kilimanjaro.

Pia, watahiniwa 79,499 (7.2%) waliochagua kipotoshi *B, Kulima kandokando ya milima* hawakuwa na maarifa ya vitendo vya kutunza mazingira. Kulima kandokando ya milima husababisha kupungua kwa uoto wa asili, na matokeo yake ni kuongezeka kwa joto hatimaye kuyeyusha theluji.

Vile vile, watahiniwa 37,392 (3.4%) walichagua *kipotoshi D, Uvunaji ovyo wa misitu.* Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu njia bora za kutunza mazingira. Uvunaji ovyo wa misitu hupunguza au kumaliza misitu kwa kasi kubwa, na matokeo yake ni kukosa mvua ambayo husababisha kutokea kwa ukame. Ukame wa muda mrefu husababisha kuongezeka kwa joto ambalo huyeyusha theluji. Pia, watahiniwa 46,436 (4.2%) waliochagua kipotoshi *E, Kufuga mifugo mingi katika eneo dogo* hawakuwa na maarifa kuhusu kuharibiwa kwa uoto unaopatikana katika eneo hilo kutokana na kufuga mifugo mingi kinyume na uwezo wa eneo husika. Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 2 umeoneshwa katika Chati Na. 1.




**Chati Na. 1**: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 2*

**Swali la 3:** Mtaalamu wa masuala ya mazingira aliwaasa wanakijiji waishio kando ya mto Mzinga kuacha tabia ya uharibifu na uchafuzi wa chanzo cha maji. Je, ni vitendo gani aliwashauri kuviacha?

A Kupanda miti, kuchoma misitu na kutupa taka katika mto

B Kulisha mifugo, kupanda nyasi na kutupa taka katika mto

C Umwagiliaji, kutengeneza matuta na kutiririsha maji taka.

D Kulima, kulisha mifugo na kukata miti

E Kuchakata malighafi, kuoga na kupozea mitambo

**Jedwali Na. 2: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 230,933 | 170,603 | 184,560 | 337,221 | 165,628 | 18,854 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 20.8 | 15.4 | 16.7 | 30.4 | 15.0 | 1.7 |

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubaini shughuli za binadamu zinazochangia uharibifu wa mto Mzinga. Kwa ujumla ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa hafifu kwani watahiniwa 337,221 (30.4%) walichagua jibu sahihi *D*, *Kulima, kulisha mifugo na kukata miti*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu shughuli za kibinadamu zinazoweza kuharibu mazingira na kuchafua maji. Kilimo hutumia mbolea na madawa, ulishaji wa mifugo husababisha kupotea kwa uoto wa asili, na ukataji miti husababisha kupungua kwa mvua. Vitendo hivi kwa ujumla husababisha uharibifu wa mazingira na uchafuzi wa vyanzo vya maji.

Hata hivyo, watahiniwa 230,933 (20.8%) walivutiwa na kipotoshi *A*, *Kupanda miti, kuchoma misitu na kutupa taka katika mto.* Watahiniwa hawa walipaswa kuelewa kuwa kupanda miti huchangia upatikanaji wa mvua, hivyo kusababisha kuongezeka kwa maji. Hivyo wanakijiji hawapaswi kuacha kitendo hicho.

Pia, watahiniwa 170,603 (15.4%) walichagua kipotoshi *B*, *Kulisha mifugo, kupanda nyasi na kutupa takataka katika mto.* Vitendo vilivyotajwa hapa husababisha uchafuzi wa mazingira isipokuwa kitendo cha kupanda nyasi. Hivyo watahiniwa hao hawakujua kuwa kupanda nyasi kunasaidia kuhifadhi uoto ambao huifadhi chanzo cha mto.

Watahiniwa wengine 184,560 (16.7%) walichagua kipotoshi *C, Umwagiliaji, kutengeneza matuta na kutiririsha maji taka.* Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu shughuli za binadamu zinazoweza kuharibu na kuchafua mto. Hivyo hawakutambua kuwa umwagiliaji ukifanyika vizuri hauwezi kuathiri vyanzo vya maji. Pia, utengenezaji wa matuta husaidia kuzuia mmomonyoko wa udongo na kuzuia uchafuzi wa maji.

Aidha, watahiniwa 165,628 (15.0%) waliochagua kipotoshi *E*, *Kuchakata malighafi, kuoga na kupozea mitambo* walihusianisha athari za viwanda katika uchafuzi wa mazingira, hususani uchafuzi wa vyanzo vya maji. Watahiniwa hao hawakutambua kuwa uchakataji wa malighafi na upoozaji wa mitambo hauwezi kuharibu vyanzo vya maji endapo taratibu zote zinazotakiwa kufanyika zimezingatiwa.

**Swali la 4:** Mtaalamu wa madini aliwatembelea wanafunzi wa Darasa la Saba na kuwafundisha aina mbalimbali za madini na kazi zake. Je ni madini yapi hutumika kukatia vioo?


A Dhahabu B Almasi C Fedha
D Tanzanaiti E Shaba

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubainisha madini yanayotumika kukata vioo. Ufaulu katika swali hili ulikuwa wa kiwango cha wastani kwani watahiniwa 553,986 (50.0%) walichagua jibu sahihi *B, Almas*i. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu aina, sifa na matumizi ya madini. Hivyo, waliweza kubaini kuwa almasi ni madini magumu kuliko yote duniani na hutumika kukata vitu vigumu ikiwemo vioo.

Hata hivyo, watahiniwa 85,995 (7.8%) walichagua kipotoshi *A*, *Dhahabu*. Uchaguzi huu umesababishwa na kutotambua kwao matumizi ya madini mbalimbali. Aidha, uwepo wa maeneo ya uchimbaji wa dhahabu katika mikoa ya Geita, Shinyanga, Tabora, Mwanza, Mbeya na Tanga pamoja na makampuni makubwa ya uchimbaji madini kama Barrick, Golden Pride na Buzwagi yamefanya madini haya kufahamika zaidi miongoni mwa wanafunzi wengi na kusababisha kuchagua dhahabu kama jibu sahihi.

Watahiniwa wengine 54,984 (5.0%) waliochagua kipotoshi *C*, *Fedha* hawakuwa na uelewa kuhusu matumizi ya madini haya. Fedha hutumika kutengeneza nyaya za umeme na sarafu. Watahiniwa walihusianisha ugumu wa sarafu na baadhi ya nyaya za umeme na uwezo wa kukata vioo.

Watahiniwa 109,886 (9.9%) walichagua kipotoshi *D, Tanzanaiti.* Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu matumizi ya madini mbalimbali. Jumla ya watahiniwa 287,268 (25.9%) walichagua kipotoshi *E*, *Shaba.* Shaba hutumika kutengeneza nyaya za umeme, silaha za kivita, na vyombo vya nyumbani kama vile sahani na vikombe. Watahiniwa hao walihusianisha kimakosa matumizi haya ya shaba na uwezo wa kukata vioo. Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 4 umeoneshwa katika Chati Na. 2.




**Chati Na. 2**: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 4*

**Swali la 5:** Mzee Mahiya ni mfugaji ambaye huhamahama na idadi kubwa ya mifugo. Ni madhara yapi husababishwa na aina hii ya ufugaji?

A Mafuriko
B Kustawi kwa uoto wa asili
C Kufa kwa mifugo
D Kupotea kwa misitu
E Kuharibika kwa mazao

**Jedwali Na. 3: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 125,475 | 77,789 | 280,796 | 281,851 | 326,511 | 15,377 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 11.3 | 7.0 | 25.3 | 25.4 | 29.5 | 1.4 |

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kuchambua madhara yanayosababishwa na ufugaji wa kuhamahama. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa kiwango hafifu kwani watahiniwa 281,851 (25.4%) tu ndio waliochagua jibu sahihi *D*, *kupotea kwa misitu.* Watahiniwa walioweza kubaini jibu sahihi walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu athari za ufugaji wa kuhamahama. Athari hizi kama ukataji miti hovyo kwa ajili ya kutengeneza mazizi ya mifugo na makazi ya binadamu. Shughuli hizo huchangia kumaliza uoto wa asili na kuleta mmomonyoko wa udongo ambao husababisha kupotea kwa misitu. Hata hivyo, watahaniwa 125,475 (11.3%) walichagua kipotoshi *A*, *Mafuriko.* Watahiniwa hao walishindwa kutambua kuwa mafuriko hayasababishwi na ufugaji wa kuhamahama, bali kunyesha kwa mvua kubwa.

Watahiniwa 77,789 (7.0%) walichagua kipotoshi *B, Kustawi kwa uoto wa asili.* Watahiniwa hao walivutiwa kuchagua kwa kuwa kinyesi cha mifugo hutumika kama mbolea. Hivyo walithani pia, kuwa hutumika kurutubisha uoto wa asili. Vile vile, watahiniwa 280,796 (25.3%) walichagua kipotoshi *C*, *Kufa kwa mifugo.* Watahiniwa hao walihusianisha kutembea kwa umbali mrefu kwa mifugo na kifo. Hawakutambua kuwa mifugo mingi hufa kutokana na

kukosa maji, chakula na magonjwa na si kutembea umbali mrefu. Pia, watahiniwa 326,511 (29.5%) waliochagua kipotoshi *E*, *Kuharibika kwa mazao* walihusianisha uharibifu unaotokana na wanyama wanapokuwa kwenye malisho. Hawakufahamu kuwa uharibifu huo huweza kutokea hata kama kundi hilo la mifugo halihamihami.

**Swali la 6:** Bwawa la Nyerere ni mojawapo ya chanzo kinachotarajiwa kuzalisha nishati ya umeme wa maji nchini Tanzania. Je, bwawa hili limejengwa katika mto gani?


| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| A | Ruaha | B | Ruvuma | C | Ruvu |
| D | Rufiji | E | Pangani | | |

Mtahiniwa alitakiwa kubainisha jina la mto ambao bwawa la kuzalisha umeme la Nyerere linajengwa. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani watahiniwa 445,628 (40.2%) walichagua jibu sahihi *D*, *Rufiji.* Watahiniwa hao walitambua kuwa bwawa la Nyerere linajengwa kwenye maporomoko ya mto Rufiji. Mbali na kusoma darasani, Wanafunzi hao wamepata maarifa kupitia mijadala kuhusu ujenzi wa bwawa la Nyerere kupitia bungeni, katika vyombo vya habari na kwenye mitandao ya kijamii.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 133,174 (12.0%) walichagua kipotoshi *A, Ruaha.* Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa kuwa mto huu ni chanzo cha bwawa la kufua Umeme la Kidatu. Hivyo, watahiniwa walijibu kutokana na kukosa maarifa kuhusu mabwawa ya umeme Tanzania na vyanzo vyake.

Jumla ya watahiniwa 275,325 (24.9%) waliochagua kipotoshi *B, Ruvuma* hawakuwa na maarifa kuwa mto huu hautumiki kuzalisha umeme. Pia, watahiniwa 95,660 (8.6%) waliochagua kipotoshi *C, Ruvu* walikuwa na maarifa kuhusu ujenzi wa bwawa la Nyerere, lakini walishindwa kutofautisha kati ya mto huu na Rufiji kutokana na kuwa na sifa zinazokaribia kufanana. Mito hii hupatikana katika mkoa wa Pwani, pia majina yake yanakaribia kufanana.

Mbali na hao, watahiniwa 140,045 (12.6%) waliochagua kipotoshi *E, Pangani* hawakuelewa kuwa katika mto Pangani kumejengwa bwawa la kufua umeme la Hale, wakati Bwawa la Nyerere linajengwa kwenye Mto Rufiji. Watahiniwa wengine 17,967 (1.6%) hawakujibu swali hili au waliandika jibu zaidi ya moja. Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 6 umeoneshwa katika Chati Na. 3.




**Chati Na. 3**: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 6*

**Swali la 7:** Musa hutoka jasho kwa wingi wakati wa msimu wa joto. Je, utamshauri avae nguo ya rangi gani?

A Nyeupe B Nyeusi C Bluu
D Njano E Kijani

**Jedwali Na. 4: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 512,590 | 433,836 | 65,864 | 36,741 | 43,439 | 15,329 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 46.3 | 39.2 | 5.9 | 3.3 | 3.9 | 1.4 |

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kubaini rangi sahihi ya nguo inayofaa kuvaliwa wakati wa msimu wa joto. Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa ni wa kiwango cha wastani kwani jumla ya watahiniwa 512,590 (46.3%) walichagua jibu sahihi *A, Nyeupe.* Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha yaliyowawezesha kutambua kuwa rangi nyeupe zinaakisi mionzi ya

jua. Kitendo hiki hupunguza kiwango cha miali ya jua ambayo ingeufikia mwili, hivyo kupunguza joto.

Jumla ya watahiniwa 433,836 (39.2%) waliochagua kipotoshi *B, Nyeusi* hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu rangi hii kuwa ina tabia ya kusharabu mwanga wa jua. Hali hii husababisha mionzi ya jua kupenya na kuufikia mwili, hivyo kusababisha kuhisi joto kali. Watahiniwa hao walifikiri kitendo hiki hupunguza joto la mwili. Kipotoshi *C*, *Bluu* kiliwavutia watahiniwa 65,864 (5.9%) ambao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu tabia na matumizi sahihi ya tofauti za nguo kutokana na hali, majira na nyakati.

Pia, watahiniwa 36,741 (3.3%) waliochagua kipotoshi *D*, *Njano* hawakuwa na maarifa kuhusu uwezo wa rangi hii kusharabu mwanga wa jua. Kitendo cha kusharabu mwanga wa jua husababisha joto la mwili kuongezeka. Vile vile, watahiniwa 43,439 (3.9%) waliochagua kipotoshi *E*, *Kijani* hawakuwa na maarifa kuhusu tabia za rangi katika kusharabu au kuakisi mwanga wa jua. Watahiniwa walijibu kwa kuzingatia hali ya mazingira kwani yametawaliwa na miti yenye rangi ya kijani, na hutumia miti kujikinga na jua. Watahiniwa 15,329 (1.4%) hawakujibu swali hili au walichagua jibu zaidi ya moja.

**Swali la 8:** Kuongezeka kwa joto duniani kunakosababishwa na shughuli za kibinadamu kama vile uchomaji wa misitu, uzalishaji wa gesiukaa kutoka viwandani na uchomaji wa mkaa husababisha madhara yafuatayo **isipokuwa**

A kuyeyuka kwa theluji katika mlima Kilimanjaro.
B kupotea kwa bayoanuai.
C kuongezeka kwa kina cha maji ya bahari.
D kuongezeka kwa uoto wa asili.
E kutokea kwa ukame.


Mtahiniwa alitakiwa kubainisha jambo ambalo halisababishwi na ongezeko la joto duniani. Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa cha wastani kwani watahiniwa 527,549 (47.6%) walichagua jibu sahihi *D*, *Kuongezeka kwa uoto wa asili.* Watahiniwa walioweza kubaini jibu sahihi walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya sababu za mabadiliko ya hali ya hewa. Hata hivyo, watahiniwa

119,314 (10.8%) waliochagua kipotoshi *A, Kuyeyuka kwa theluji* hawakutambua kuwa theluji katika Mlima Kilimanjaro inayeyuka kutokana na kuongezeka kwa joto duniani.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 89,481 (8.1%) walichagua kipotoshi *B, Kupotea kwa bayoanuai.* Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa ongezeko la joto huharibu msawazo asilia na ikolojia katika mazingira, na hivyo kusababisha vifo vya viumbe. Watahiniwa hao hawakuelewa uhusiano uliopo baina ya kuongezeka kwa joto na kupotea na bayoanuai.

Kipotoshi *C, Kuongezeka kwa kina cha maji ya bahari* kilichaguliwa na watahiniwa 227,847 (20.6%). Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa kuongezeka kwa joto husababisha kuyeyuka kwa theluji iliyopo kwenye ncha za dunia. Theluji hiyo inapoyeyuka, huchangia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa maji katika bahari. Watahiniwa hao walijibu swali kwa kuhusianisha tukio hili na faida ya kupata maji mengi kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

Vile vile, watahiniwa 128,302 (11.6%) walichagua kipotoshi *E, Kutokea kwa ukame.* Chaguo hilo halikuwa sahihi kwani kuongezeka kwa joto husababisha mvua kutonyesha kwa muda mrefu na kusababisha kutokea kwa ukame. Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 8 umeoneshwa katika Chati Na. 4.




**Chati Na. 4**: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 8*

**Swali la 9:** Mtaalamu wa hali ya hewa alisoma kiwango cha juu cha jotoridi la siku kama nyuzi joto $42^oC$ na kiwango cha chini $20^oC$. Upi ni utofauti wa kiwango cha jotoridi kwa siku?

A $62^0C$ B $62^0F$ C $22^0F$
D $22^0C$ E $134^0F$

**Jedwali Na. 5: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 178,320 | 128,033 | 205,499 | 503,613 | 74,762 | 17,572 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 16.1 | 39.2 | 18.6 | 45.5 | 6.7 | 1.6 |

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kukokotoa tofauti ya kiwango cha joto kwa siku. Kiwango cha juu cha joto kilikuwa nyuzi joto $42^oC$ na kiwango cha chini kilikuwa nyuzi joto $20^oC$. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani watahiniwa 503,613 (45.5%) walichagua jibu sahihi *D*, *$22^0C$.* Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya upimaji wa vipengele vya hali ya hewa ikiwemo jotoridi. Pia walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu vitendo vya hesabu kwa kuwa waliweza kuchukua kiwango cha juu cha joto kwa siku ($42^oC$) kutoa kiwango cha chini cha joto la siku ($20^oC$) ili kupata tofauti ya jotoridi kwa siku hiyo.

Jumla ya watahiniwa 178,320 (16.1%) waliochagua kipotoshi *A, 62 $^0C$* hawakuwa na maarifa ya kutosha kufahamu namna ya kupata utofauti wa kiwango cha joto kwa siku. Hivyo, walijumlisha jotoridi la juu ($42^oC$) na joto la chini ($20^oC$) wakapata 62 $^0C$ ambalo sio jibu sahihi.

Kwa upande wa watahiniwa 128,033 (39.2%) waliochagua kipotoshi *B, 62 $^0F$,* hawakuwa na maarifa ya vitendo vya kuhesabu ambapo walikokotoa jumla ya jotoridi la chini na la juu. Hivyo walishindwa kutambua kuwa walitakiwa kukokotoa utofauti wa joto la siku. Watahiniwa hao walishindwa pia kutambua kuwa jotoridi la siku lilikuwa kwenye kizio cha sentigredi na si Farenheiti.

Vile vile, watahiniwa 205,499 (18.6%) waliochagua kipotoshi *C,* $22^0$*F,* walikuwa na maarifa ya vitendo vya hesabu kwa kuwa walikokotoa utofauti wa jotoridi. Hata hivyo, walishindwa kutambua kizio sahihi ambapo walichagua kizio cha Farenheiti badala ya sentigredi.

Hata hivyo, watahiniwa 74,762 (6.7%) walichagua kipotoshi *E, 134* $^0$*F.* Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kuwawezesha kupata jibu kwa kuwa hakuna vitendo vya hesabu vinavyoweza kuleta jibu la jotoridi hilo iwe kwa kutoa, kujumllisha au kwa kubadili kizio cha sentigredi kwenda farenheiti.

**Swali la 10:** Wanafunzi wa Darasa la Nne walijifunza juu ya uhusiano uliopo kati ya jua, mimea na maji juu ya uso wa dunia. Yapi ni matokeo ya uhusiano huo?

A Kutokea kwa upepo
B Kufanyika kwa mvua
C Kuganda kwa maji
D Kutokea kwa kimbunga
E Kuyeyuka kwa barafu


Mtahiniwa alitakiwa kubaini matokeo ya uhusiano uliopo kati ya jua, mimea na maji juu ya uso wa dunia. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa ni wa wastani kwani watahiniwa 562,323 (50.8%) walichagua jibu sahihi *B*, *Kufanyika kwa mvua*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mvua inavyotokea. Jua linapowaka juu ya uso wa dunia huchemsha maji yaliyoko ardhini, kwenye majani ya mimea, na kwenye vyanzo vya maji na kufanya hewa kuwa nyepesi. Hewa hiyo hubeba mvuke kutoka kwenye mimea kwa njia iitwayo transpiresheni, na mvuke kutoka kwenye vyanzo vya maji kwa njia ya mvukizo. Baada ya matendo hayo, hewa hupata joto na kuwa nyepesi. Hewa hiyo hubeba unyevu na kupaa angani ambapo jotoridi hupungua na kujikusanya hadi kufikia kiwango cha umande. Baadaye hugeuka kuwa mawingu mazito ambayo hudondoka chini kama mvua.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 154,677 (14.0%) waliochagua kipotoshi *A, Kutokea kwa upepo* hawakuwa na uelewa wa namna upepo unavyotokea. Watahiniwa hao walitakiwa kuelewa kwamba, upepo hutokea kutokana na utofauti wa mgandamizo wa hewa kati

ya sehemu moja na nyingine. Pia, ongezeko la joto husababisha hewa kutanuka na kuwa nyepesi hivyo kupaa.

Jumla ya watahiniwa 112,891 (10.2%) walichagua kipotoshi *C*, *Kuganda kwa maji.* Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa kuganda kwa maji ni matokeo ya kushuka kwa kiwango cha jotoridi hadi kufikia nyuzi joto $0^{0}$C. Hivyo, hakuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya jua, mimea na maji.

Pia, watahiniwa 83,979 (7.6%) waliochagua kipotoshi *D*, *Kutokea kwa kimbunga* hawakuelewa kuwa kimbunga ni matokeo ya mawimbi makubwa ya bahari. Watahiniwa 175,871 (15.9%) waliochagua kipotoshi *E, Kuyeyuka kwa barafu,* hawakutambua kuwa hayo ni matokeo ya kuongezeka kwa joto duniani. Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 10 umeoneshwa katika Chati Na. 5.




**Chati Na. 5**: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 10*

**Swali la 11:** Katika uso wa Dunia kuna pepo zinazovuma kutoka eneo moja kwenda jingine. Je, ni upepo gani unavuma kutoka Kusini kuelekea Kaskazini?

| | | | |
|---|---|---|---|
| A | Upepo wa Kusi | B | Upepo wa Kaskazini |
| C | Upepo mkavu | D | Upepo wa Magharibi |
| E | Upepo unyevu | | |

**Jedwali Na. 6: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 489,700 | 173,782 | 166,760 | 125,379 | 131,994 | 20,184 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 44.2 | 15.7 | 15.1 | 11.3 | 11.9 | 1.8 |

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubaini jina la upepo unaovuma kutoka upande wa Kusini kuelekea Kaskazini. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani watahiniwa 489,700 (44.2%) walichagua jibu sahihi *A, Upepo wa Kusi.* Watahiniwa hao, walikuwa na maarifa ya kutosha kuwa jina la upepo hutegemea upande unapotokea.


Jumla ya watahiniwa 173,782 (15.7%) walichagua vipotoshi *B*, *Upepo wa Kaskazini,* na kipotoshi *D*, *Upepo wa Magharibi* kilichaguliwa na watahiniwa 125,379 (11.3%). Watahiniwa hao hawakuwa na uelewa kuhusu majina ya upepo yanavyopatikana. Majina ya upepo hutajwa kulingana na upepo unakotokea, na si unakoelekea. Hivyo, upepo unaovuma kutoka kusini kuelekea kaskazini hauwezi kuwa upepo wa kaskazini wala magharibi.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 166,760 (15.1%) walichagua kipotoshi *C*, *Upepo mkavu,* na watahiniwa 131,994 (11.9%) walichagua kipotoshi *E*, *Upepo unyevu.* Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu upepo katika sura ya dunia. Walitakiwa kujua kuwa majina ya upepo hutegemea uelekeo wake zinapovuma. Pia, hawakuelewa kuwa upepo mkavu hutokea kwenye maeneo yenye ukame, na upepo unyevu huvuma kutoka kwenye maeneo ya maji.

**Swali la 12:** Tanzania ina makabila mengi yenye mila nzuri na potofu. Ni mila ipi yenye madhara kwa jamii ?

A Kuruhusu wanawake wajawazito kula mayai
B Kukeketa watoto wa kike
C Kufundisha wavulana na wasichana kuhusu maadili
D Kutahiri wavulana
E Kuwapa wanawake haki sawa na wanaume

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubaini mila potofu yenye madhara kwa jamii. Ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwani watahiniwa 964,363 (87.1%) waliweza kuchagua jibu sahihi *B*, *Kukeketa watoto wa kike.* Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu madhara ya ukeketaji kwa wanawake kuwa ni kupoteza damu nyingi wakati wa kukeketwa, au wakati wa kujifungua na huweza kusababisha kifo. Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 12 umeoneshwa katika Chati Na. 6.




**Chati Na. 6:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 15*

Kwa upande mwingine, jumla ya watahiniwa 31,704 (2.9%) waliochagua kipotoshi *A*, *Kuruhusu wanawake wajawazito kula mayai* hawakuwa na uelewa juu ya mila zisizofaa katika jamii. Watahiniwa hao walipaswa kuelewa kuwa ulaji wa mayai huupatia

mwili wa mama mjamzito protini na makuzi yenye afya kwa mtoto aliyeko tumboni.

Hata hivyo, watahiniwa 39,888 (3.6%) waliochagua kipotoshi *C, Kufundisha wavulana na wasichana kuhusu maadili,* hawakujua umuhimu wa kufundisha maadili kwa vijana. Watahiniwa hao walipaswa kuelewa kuwa kufundisha wavulana na wasichana maadili husaidia kujenga jamii bora inayokubalika na kutekeleza majukumu mbalimbali kwa kuzingatia uwazi, ukweli na kusimamia haki, na sio kuchochea mila potofu.

Pamoja na hayo, watahiniwa 30,123 (2.7%) walichagua kipotoshi *D*, *Kutahiri wavulana.* Uchaguzi wa kipotoshi hicho unathibitisha kuwa watahiniwa hao walikuwa na uelewa mdogo kuhusu tohara kwa wavulana. Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa, tohara kwa wavulana inakubalika katika jamii kutokana na kumfanya mvulana kuwa nadhifu, na kumsaidia kupunguza maambukizi ya magonjwa yakiwemo ya zinaa.

Vilevile, jumla ya watahiniwa 30,277 (2.7%) walichagua kipotoshi *E*, *Kuwapa wanawake haki sawa na wanaume.* Watahiniwa hao walikosa maarifa ya kutosha kwa kuwa walishindwa kuelewa kwamba kuwapa wanawake haki sawa na wanaume kunasisitiza kulinda na kuheshimu haki za binadamu. Hivyo, inapaswa kudumishwa sio kuondolewa kama mila potofu.

**Swali la 13:** Kila jamii nchini Tanzania ina michezo yake ya asili kulingana na mazingira, muda na utamaduni. Ipi ni mifano ya michezo hiyo?

A Mpira wa miguu, ngumi na kukimbia
B Kukimbia, kuogelea na mpira wa miguu
C Kurusha mkuki, kuruka kamba na kukimbia
D Mpira wa miguu, pete na kuogelea
E Mpira wa kikapu, miguu na pete

**Jedwali Na. 7: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Machaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahinwa | 175,753 | 118,558 | 497,872 | 66,333 | 232,648 | 16,635 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 15.9 | 10.7 | 44.9 | 6.0 | 21.0 | 1.5 |

Swali hili lilipima uwezo wa mtahiniwa kubaini aina za michezo ya asili kulingana na mazingira, muda na utamaduni. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa ni wastani kwani watahiniwa 497,872 (44.9%) walichagua jibu sahihi *C*, *Kurusha mkuki, kuruka kamba na kukimbia.* Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu michezo ya asili. Walikuwa na uelewa kuwa michezo ya asili ni ile inayotumia zana za asili kama vile mikuki, pinde na mishale na kamba. Michezo ya kigeni hutumia zana za kisasa zilizoingizwa kutoka nchi za nje kama mipira.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 609,927 (55.1%) walichagua kipotoshi *A*, *Mpira wa miguu, ngumi na kukimbia, B*, *Kukimbia, kuogelea na mpira wa miguu, D*, *Mpira wa miguu, pete na kuogelea* na *E*, *Mpira wa kikapu, miguu na pete.* Uchaguzi wa vipotoshi hivyo unaashiria kuwa watahiniwa wengi hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu michezo ya jadi/asili ya jamii za Tanzania. Watahiniwa hao walisukumwa kuchagua vipotoshi hivyo kutokana na umaarufu wa michezo hiyo katika jamii zao hususani mpira wa miguu na ngumi.

**Swali la 14:** Ni kwa namna gani jamii inaweza kukabiliana na tamaduni zilizopitwa na wakati?

A Kudumisha umoja wa kitaifa
B Kudumisha misingi ya uzalendo
C Kuwa na misingi ya mila na desturi zinazofanana
D Kupenda jamii na taifa
E Kufanya majadiliano na jamii inayohusika

**Jedwali Na. 8: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Machaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahinwa | 191,607 | 204,237 | 316,462 | 96,349 | 282,191 | 16,953 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 17.3 | 18.4 | 28.6 | 8.7 | 25.5 | 1.5 |

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubaini namna ya kupambana na tamaduni zilizopitwa na wakati. Ufaulu katika swali hili ulikuwa hafifu kwani watahiniwa 282,191 (25.5%) tu ndio walioweza kuchagua jibu sahihi *E*, *Kufanya majadiliano na jamii inayohusika*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu namna ya kukabiliana na tamaduni zilizopitwa na wakati. Aidha, watahiniwa hao waliweza kutambua kuwa majadiliano ni muhimu ili jamii iweze kutambua umuhimu wa kuacha mila zilizopitwa na wakati; na kutafuta njia mbadala ya kutatua changamoto zilizowakabili hapo awali.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 191,607 (17.3%) waliochagua kipotoshi *A, Kudumisha umoja wa kitaifa* hawakuwa na umahiri wa kutosha. Walishindwa kuelewa kuwa kudumisha umoja wa kitaifa ni njia muhimu kwa jamii katika kuimarisha maendeleo ya taifa kisiasa, kijamii na kiuchumi; na sio njia ya kukabiliana na tamaduni zilizopitwa na wakati.

Hata hivyo, watahiniwa 204,237 (18.4%) walichagua kipotoshi *B, Kudumisha misingi ya uzalendo.* Watahiniwa hawa hawakuelewa kwamba misingi ya uzalendo ni ya muhimu kwa kila mmoja wetu kwa sababu inajenga jamii iliyo bora. Vilevile, watahiniwa 316,462 (28.6%) waliovutiwa na kipotoshi *C*, *Kuwa na misingi ya mila na desturi zinazofanana* hawakuwa na umahiri wa kutosha juu ya njia za kukabiliana na tamaduni zisizofaa. Kuwa na misingi ya mila na desturi zinazofanana hakuhusiani moja kwa moja na kusaidia jamii kuondokana na tamaduni zilizopitwa na wakati.

Pamoja na hayo, watahiniwa 96,349 (8.7%) walichagua kipotoshi *D*, *Kupenda jamii na taifa*. Uchaguzi wa kipotoshi hicho unathibitisha kuwa watahiniwa hao walikuwa na uelewa mdogo kuhusu namna ya kukabiliana na tamaduni zilizopitwa na wakati. Watahiniwa hao

walipaswa kuelewa kwamba kupenda jamii na taifa ni sifa za mashujaa. Aidha, kuwa shujaa sio sababu ya kumfanya mtu kupinga tamaduni zilizopitwa na wakati katika jamii.

**Swali la 15:** Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua umuhimu wa michezo kama nyenzo ya kuburudisha na kuwaunganisha raia wake. Ni taasisi ipi inayohusika zaidi katika kusimamia na kuendeleza michezo nchini Tanzania?

A Baraza la Sanaa la Taifa
B Baraza la Kiswahili la Taifa
C Baraza la Michezo ya Ridhaa la Taifa
D Baraza la Michezo la Taifa
E Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania

**Jedwali Na. 9: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Machaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 277,721 | 83,675 | 152,102 | 426,575 | 154,922 | 12,876 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 25.10 | 7.60 | 13.70 | 38.50 | 14.00 | 1.20 |

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubaini taasisi inayohusika zaidi katika kusimamia na kuendeleza michezo nchini Tanzania. Kwa ujumla, kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa cha wastani. Watahiniwa 454,577 (41.0%) ndio waliweza kuchagua jibu sahihi *D*, *Baraza la Michezo la Taifa.* Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu taasisi inayohusika katika kusimamia, kukuza na kuendeleza michezo nchini Tanzania.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 282,845 (25.5%) waliochagua *A*, *Baraza la Sanaa la Taifa* hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Baraza la Sanaa la Tanzania (BASATA) na vyombo mbalimbali na majukumu yake. Watahiniwa hao walitakiwa kujua kwamba BASATA ilianzishwa kwa madhumuni ya kufufua, kuendeleza na kukuza kazi za sanaa za asili ya Mtanzania kama vile muziki, filamu, maigizo, uchongaji na sanaa ya uchoraji.

Pamoja na hayo, watahiniwa 74,792 (6.8%) waliochagua kipotoshi *B*, *Baraza la Kiswahili la Tanzania* (BAKITA) hawakuelewa kwamba BAKITA ilianzishwa na kupewa dhamana ya kusimamia na kukuza lugha ya Kiswahili, na sio kusimamia na kuendeleza michezo nchini Tanzania. Hata hivyo, watahiniwa 137,128 (12.4%) waliochagua kipotoshi *C*, *Baraza la Michezo ya Ridhaa la Taifa,* walikuwa na uelewa mdogo kuhusu Baraza hilo. Watahiniwa hao walipaswa kuelewa kuwa taasisi hii husimamia michezo ya kujitolea mfano wanyanyua vitu vizito, ngumi na riadha.

Vilevile, jumla ya watahiniwa 146,034 (13.2%) walichagua kipotoshi *E*, *Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania.* Watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa kazi ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania ni kusimamia mchezo wa mpira wa miguu tu.

**Swali la 16:** Yafuatayo huweza kutokea kwa taifa linalokuza utamaduni wake **isipokuwa**

A kudumisha misingi ya uzalendo
B kuiga tamaduni za kigeni
C kudumisha umoja
D kulinda asili yake
E kuwepo kwa uhusiano mzuri katika jamii.

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubaini jambo lisiloweza kutokea kwa taifa linalokuza utamaduni wake. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwani watahiniwa 846,957 (76.5%) walichagua jibu sahihi *B, Kuiga tamaduni za kigeni*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa kuwa kuiga tamaduni za kigeni husababisha mmomonyoko wa maadili. Kwa mfano, uvaaji wa mavazi ya kigeni, kula vyakula vya kigeni na kucheza michezo ya kigeni.

Aidha, watahiniwa 55,107 (6.5) walichagua kipotoshi *A*, *Kudumisha misingi ya uzalendo.* Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuwa uzalendo una mchango mkubwa katika kukuza na kuimarisha utamaduni wa jamii husika. Watahiniwa hao walipaswa kuelewa kwamba uzalendo ukifundishwa kwa watoto utasaidia kukuza utamaduni katika jamii.

Jumla ya watahiniwa 59,532 (5.4%) walichagua kipotoshi *C, Kudumisha umoja.* Chaguo hilo halikuwa sahihi kwa sababu kudumisha umoja huchangia kuifanya jamii kuwa na mwelekeo mmoja katika kukuza utamaduni wao. Watahiniwa 117,036 (10.6%) walichagua kipotoshi *D*, *Kulinda asili yake.* Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa kulinda asili yake ni moja ya njia ya kukuza utamaduni wa jamii fulani.

Kipotoshi *E*, *Kuwepo kwa uhusiano mzuri katika jamii* kilichaguliwa na watahiniwa 57,497 (5.5%). Chaguo hilo halikuwa sahihi kwa sababu, kuwapo kwa uhusiano mzuri katika jamii husaidia kukuza utamaduni wa jamii husika. Watahiniwa hao walipaswa kuelewa kwamba, kuwepo kwa uhusiano mzuri katika jamii ni sehemu ya utamaduni.

**Swali la 17:** Kasuku anaipenda nchi yake, ana moyo wa kujitoa kwa Taifa lake na ni mtunzaji mzuri wa rasilimali za Taifa. Kasuku anaweza kuwa na sifa ipi kwa taifa lake?

A Mlinzi wa rasilimali za nchi
B Mzalendo kwa taifa lake
C Mtunzaji wa miiko ya jamii
D Mlinda usalama wa jamii
E Msimamizi wa umoja wa wananchi

**Jedwali Na. 10: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| **Machaguo** | **A** | **B*** | **C** | **D** | **E** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 117,439 | 846,957 | 46,751 | 44,350 | 42,058 | 10,244 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 10.6 | 76.5 | 4.2 | 4.0 | 3.8 | 0.9 |

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kutambua sifa za mtu anayeipenda nchi yake, mwenye moyo wa kujitoa kwa taifa lake pamoja na kulinda rasilimali za taifa. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwani watahiniwa 846,957 (76.5%) walichagua jibu sahihi *B, Mzalendo kwa taifa lake*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu uzalendo, kuwa ni hali ya kuipenda nchi,

kuitumikia na kulinda rasilimali zake. Jumla ya watahiniwa 117,439 (10.6%) walichagua kipotoshi *A*, *Mlinzi wa rasilimali za nchi.* Chaguo hilo halikuwa sahihi kwa sababu kazi ya ulinzi wa rasilimali za nchi ni jukumu la kila raia katika nchi.

Hata hivyo, watahiniwa wengine 46,751 (4.2%) walivutiwa na kipotoshi *C*, *Mtunzaji wa miiko ya jamii.* Watahiniwa hao, walishindwa kutambua kuwa utunzaji wa miiko ya jamii pekee haumsaidii mtu kuipenda nchi yake, kuwa na moyo wa kujitolea kwa taifa lake, na kuwa mtunzaji mzuri wa rasilimali za taifa. Vilevile, watahiniwa 44,350 (4.0%) waliochagua kipotoshi *D*, *Mlinda usalama wa jamii* walishindwa kuelewa kuwa jukumu la kulinda usalama wa jamii ni kazi ya kila raia wakishirikiana na jeshi la polisi.


Pia, watahiniwa 42,058 (3.8%) waliochagua kipotoshi *E*, *Msimamizi wa umoja wa nchi* hawakuwa na uelewa kuwa mtu anapokuwa mzalendo katika utendaji wake, pia atakuwa anasimamia umoja wa nchi. Japo hii sio sifa pekee inayomfanya mtu kuwa mzalendo.

**Swali la 18:** Katika mapambano ya kudai uhuru wa Tanganyika, vyama vingi vilishiriki kwa malengo tofauti. Ni chama gani kiliungwa mkono na serikali ya kikoloni ili kukidhoofisha chama cha TANU?

A Tanganyika African Association (TAA)
B Zanzibar and Pemba People’s Party (ZPPP)
C Afro Shirazi Party (ASP)
D African National Congress (ANC)
E United Tanganyika Party (UTP)

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubaini chama kilichoungwa mkono na serikali ya kikoloni ili kukidhoofisha chama cha TANU. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa hafifu kwani watahiniwa 259,289 (23.4%) tu ndio waliweza kuchagua jibu sahihi *E*, *United Tanganyika Party (UTP*). Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu vyama vya siasa vilivyoanzishwa Tanganyika kabla la uhuru. Watahiniwa hao walielewa kuwa chama *UTP* kilianzishwa na Ivon Beydon mwaka 1959, na kuungwa mkono na serikali ya kikoloni ya Uingereza kwa lengo la kuidhoofisha TANU katika juhudi zake za

kupigania uhuru wa Tanganyika. Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 18 umeoneshwa katika Chati Na. 7.




**Chati Na. 7:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 18*

Jumla ya watahiniwa 226,864 (20.5%) waliochagua kipotoshi *A*, *Tanganyika African Association (TAA)* hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu uhuru wa Tanganyika ulivyopatikana. TAA kilibadilishwa kuwa TANU mwaka 1954. Hivyo, hakikuungwa mkono na serikali ya kikoloni ili kukidhoofisha chama cha TANU.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 137,087 (12.4%) waliochagua kipotoshi *B*, *Zanzibar and Pemba People's Party (ZPPP)* hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu harakati ya ukombozi wa Tanzania. Watahiniwa hao walipaswa kuelewa ZPPP iliundwa mwaka 1959 na Washirazi chini ya uongozi wa Mohamed Shamte, baada ya kutoelewana kwa viongozi ndani ya chama cha ASP. Chama hiki kiliungwa mkono na serikali ya Uingereza kwa lengo la kupinga harakati za chama cha ASP za kutetea uhuru wa Zanzibar, na sio kuipinga TANU Tanganyika.

Hata hivyo, watahiniwa 271,446 (24.5%) waliochagua kipotoshi *C*, *Afro-Shiraz Party (ASP)* walishindwa kuelewa kuwa chama cha ASP kiliundwa mwaka 1957 huko Zanzibar kwa lengo la kuondoa ukoloni,

utawala wa Waarabu na Sultani; na sio kuidhoofisha TANU Tanganyika.

Vilevile, watahiniwa 197,898 (17.9%) waliochagua kipotoshi *D*, *African National Congress (ANC*), hawakutambua kuwa chama cha ANC hakikuungwa mkono na wazungu kuidhoofisha TANU, ingawa kilianzishwa baada ya kutokea kutoelewana ndani ya TANU.

**Swali la 19:** Jumuiya ya Afrika Mashariki ina makao makuu yake ambapo taasisi zake zote huwepo, na kazi muhimu zote hufanyika hapo. Je, makao makuu yanapatikana wapi?

A Mombasa nchini Kenya
B Kigali nchini Rwanda
C Juba nchini Sudan Kusini
D Entebbe nchini Uganda
E Arusha nchini Tanzania

**Jedwali Na. 11: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Machaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 175,209 | 79,646 | 151,652 | 64,816 | 620,720 | 15,756 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 15.8 | 7.2 | 13.7 | 5.9 | 56.0 | 1.4 |

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubaini sehemu yaliko makao makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wastani kwani watahiniwa 620,720 (56.0%) tu ndio waliweza kuchagua jibu sahihi *E*, *Arusha nchini Tanzania.* Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu yalipo makao makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 175,209 (15.8%) walichagua kipotoshi *A*, *Mombasa nchini Kenya.* Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki. Watahiniwa hao walichagua Mombasa kwa sababu ni mji wa kibiashara, na wa pili kwa ukubwa nchini Kenya.

Pamoja na hayo, watahiniwa 79, 646 (7.2%) walichagua kipotoshi *B*, *Kigali nchini Rwanda.* Uchaguzi wa kipotoshi hicho unathibitisha kuwa watahiniwa hao walikuwa na uelewa mdogo kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki. Watahiniwa hao walipaswa kuelewa kuwa, Kigali ni mji mkuu wa Rwanda. Rwanda ilijiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 2007, miaka saba baada ya kuundwa upya kwa Jumuiya hiyo mwaka 2000 hivyo isinge kuwa rahisi makao makuu ya Jumuiya hiyo kuwepo Rwanda.

Hata hivyo, watahiniwa 151,652 (13.7%) walichagua kipotoshi *C*, *Juba nchini Sudani Kusini.* Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuwa Sudan Kusini ni mwanachama mpya wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Sudan Kusini ilijiunga na Jumuiya hiyo mwaka 2016 miaka mitano tu baada ya kupata uhuru kutoka Sudan, hivyo isingekuwa rahisi makao makuu ya Jumuia hiyo kuwepo Sudan. Vilevile, jumla ya watahiniwa 64,816 (5.9%) walichagua kipotoshi *D*, *Entebe nchini Uganda.* Watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa kutosha kwamba Entebe sio makao makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki; bali ni mji wa kibiashara na wa pili kwa ukubwa nchi Uganda.

Swali **la 20:** Licha ya kugawanywa kwa Bara la Afrika katika mkutano wa Berlin wa mwaka 1884 hadi 1885, Afrika iligawanywa tena baada ya vita ya kwanza ya dunia miongoni mwa mataifa ya Ulaya **isipokuwa**

A Ufaransa B Italia

C Ubelgiji D Ureno

E Ujerumani

**Jedwali 12: Idadi na wastani wa watahiniwa katika kila chaguo**

| Machaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 122,919 | 507,353 | 175,872 | 119,713 | 167,956 | 13,986 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 11.1 | 45.8 | 15.9 | 10.8 | 15.2 | 1.3 |

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubaini taifa la Ulaya ambalo halikupata koloni barani Afrika baada ya vita kuu vya kwanza vya

dunia. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa hafifu kwani ni watahiniwa 167,956 (15.2%) tu ndio walichagua jibu sahihi *E*, *Wajerumani.* Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuwa baada ya vita kuu vya kwanza vya dunia, Ujerumani ilinyang’anywa makoloni yake yote barani Afrika ikiwemo Tanganyika. Makoloni hayo yaliwekwa chini ya uangalizi wa mataifa mengine ya Ulaya. Hii ni kwasababu Ujerumani ilituhumiwa kusababisha vita hivyo, na moja ya adhabu ilikuwa ni kuyaachia makoloni yake yote kwa mataifa mengine ya Ulaya.

Jumla ya watahiniwa 122,919 (11.5%) walivutiwa na kipotoshi *A*, *Ufaransa.* Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuwa taifa la Ufaransa ni miongoni mwa mataifa ya Ulaya yaliyopata makoloni mengi barani Afrika ikiwemo Senegali, Guinea, Morocco na Tunisia. Watahiniwa hao walipaswa kuelewa kwamba hata baada ya vita kuu ya kwanza ya dunia kumalizika, Ufaransa iliendelea kuzitawala nchi hizo hadi pale nchi hizo zilipopata uhuru wake.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 507,353 (45.8%) waliochagua kipotoshi *B*, *Italia* walikuwa na uelewa mdogo kuhusu ya vita ya kwanza ya dunia. Watahiniwa hao walipaswa kuelewa kuwa nchi ya Italia ilikuwa na makoloni Afrika ikiwemo Somalia, Eritrea na Libya; na iliendelea kuyatawala hata baada ya vita ya kwanza ya dunia.

Hata hivyo, watahiniwa 175,872 (15.9%) walichagua kipotoshi *C*, *Ubelgiji.* Watahiniwa hawa walipaswa kuelewa kuwa Ubelgiji ilipata koloni moja tu ambalo ni Kongo (Kwa sasa DRC), na iliendelea kulitawala hata baada ya vita vya kwanza vya dunia hadi nchi hiyo ilipopata uhuru wake mwaka 1960.

Vilevile, watahiniwa 119,713 (10.8%) waliochagua kipotoshi *D*, *Ureno* hawakuwa na maarifa ya kutosha kuwa taifa la Ureno liliendelea kuzitawala nchi za Angola, Msumbiji, Guinea Bissau na Cape Verde hadi miaka ya 1970 wakati watawala hao waliyapa makoloni hayo uhuru wa kisiasa.

**Swali la 21:** Nelson Mandela alifungwa gerezani kwa miaka 27 lakini hakukata tamaa. Alipambana mpaka Afrika Kusini ikapata uhuru wake. Ni maelezo yapi yanamwelezea vizuri?

A Alikuwa ni shujaa aliyekuwa Rais wa Afrika Kusini kuanzia mwaka 1988 hadi 1994.

B Alikuwa ni kiongozi mzalendo aliyepambania urejeshwaji wa mfumo wa vyama vingi.

C Alikuwa Rais wa kwanza Mwafrika katika nchi ya Afrika ya Kusini mwaka 1964.

D Alikuwa ni shujaa aliyepinga ubaguzi wa rangi katika nchi ya Afrika Kusini.

E Alikuwa ni kiongozi muhimu wa mapinduzi yaliyoipatia nchi ya Afrika Kusini uhuru.

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubaini maelezo yanayomwelezea vizuri Nelson Mandela. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa hafifu kwani watahiniwa 383,566 (34.6%) tu ndio walichagua jibu sahihi *D*, *Alikuwa ni shujaa aliyepinga ubaguzi wa rangi katika nchi ya Afrika ya Kusini*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu harakati za ukombozi wa nchi ya Afrika Kusini. Aidha, walikuwa na uelewa kuwa, Nelson Mandela alikuwa na mbinu za uongozi, maono, uvumilivu na alikuwa mwana harakati aliyepigania ukombozi wa nchi yake dhidi ya utawala wa makaburu. Harakati hizi zilifanikisha Afrika Kusini kupata uhuru wake wa kidemokrasia mwaka 1994 kutoka katika utawala wa ubaguzi wa rangi wa makaburu.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 276,396 (25.8%) waliochagua kipotoshi *A*, *Alikuwa ni shujaa aliyekuwa Rais wa Afrika ya Kusini kuanzia mwaka 1988 hadi 1994,* walikuwa na maarifa kuhusu Nelson Mandela. Hata hivyo, walishindwa kutambua kuwa Mandela hakuwa rais kati *mwaka* 1988 hadi 1994. Africa Kusini ilipata uhuru wake kamili wa kidemokrasia mwaka 1994, na kuanzia kipindi hicho Mandela alianza kuongoza nchi hiyo.

Hata hivyo, watahiniwa 155,014 (14.0%) walichagua kipotoshi *B*, *Alikuwa ni kiongozi mzalendo aliyepambania urejeshwaji wa mfumo*

*wa vyama vingi.* Uchaguzi wa kipotoshi hicho unathibitisha kuwa watahiniwa hao walikuwa na uelewa mdogo kuhusu harakati za ukombozi wa nchi ya Afrika Kusini. Watahiniwa hao walipaswa kuelewa kuwa tangu enzi za ukoloni, Afrika Kusini ilikuwa na vya vingi vya siasa. Hivyo, Mandela hakupambania urejeshwaji wa mfumo wa vyama vingi.


Vilevile, watahiniwa 113,457 waliochagua kipotoshi *C*, *Alikuwa Rais wa kwanza mwafrika katika nchi ya Afrika Kusini mwaka 1964* walikuwa na maarifa kuhusu Nelson Mandela. Hata hivyo, walishindwa kutambua historia ya Afrika ya Kusini na muda ambao marais wa Afrika Kusini walihudumu.

Pia, watahiniwa 163,475 (14.8%) walichagua kipotoshi *E*, *Alikuwa kiongozi muhimu wa mapinduzi yaliyoipatia nchi ya Afrika Kusini uhuru.* Watahiniwa hao walikuwa na uelewa kuwa Nelson Mandela alikuwa kiongozi kinara katika harakati za ukombozi wa Afrika Kusini. Hata hivyo, walishindwa kuelewa kuwa Afrika Kusini haikupata uhuru wake kwa njia ya mapinduzi, bali kwa njia ya maridhiano ya kikatiba na mapambano ya kijeshi.

**Swali la 22:** Mwalimu Julius Kambarage Nyerere anatambulika kama "Baba wa Taifa" aliyestaafu kwa hiari mwaka 1985. Je, alistaafu karne ya ngapi?

A 19 B 21 C 20
D 22 E 18

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubaini karne ambayo Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alistaafu urais kwa hiari. Kwa ujumla, kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa hafifu kama inavyoonekana kwenye Chati Na. 8.




**Chati Na. 8:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 22*

Jumla ya watahiniwa 272,575 (24.6%) walichagua jibu sahihi *C, Karne ya 20*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu kiongozi huyo. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa kuhusu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na kipindi alicho acha kuwa Rais.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 390,130 (35.2%) waliochagua kipotoshi *A*, karne ya *19,* hawakuwa na maarifa kuhusu matukio mbalimbali ya kihistoria yaliyotokea Tanzania kwenye karne ya 19. Watahiniwa hao walipaswa kuelewa kuwa, katika karne ya 19 baadhi ya mataifa ya Ulaya walivamia na kuanza kutawala Tanganyika na Afrika kwa ujumla. Hivyo katika kipindi cha karne ya 19 Mwalimu Julias J.K. Nyerere hakuwa amezaliwa na hakuwa rais wa nchi inayoitwa Tanzania.

Pamoja na hayo, watahiniwa 142,014 (12.8%) walichagua kipotoshi *B*, karne ya *21.* Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu matukio ya kihistoria Tanzania. Vilevile, jumla ya watahiniwa 75,702 (6.8%) walichagua kipotoshi *D*, *karne ya 22.* Watahiniwa hao walikuwa na uelewa mdogo kuhusu kutambua wakati na matukio yanayohusiana na historia. Watahiniwa hao walishindwa kutambua kuwa tuko katika karne ya 21, hivyo basi karne ya 22 bado haijafika. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *E*, karne ya *18* hawakuwa na ufahamu kuhusu matukio ya kihistoria yaliyotokea kabla na wakati wa ukoloni Tanganyika (Tanzania).

**Swali la 23:** Vyama vingi vya siasa Afrika vilikabiliwa na matatizo yaliyoathiri juhudi katika kushiriki harakati za kupigania uhuru. Kipi kilisababisha chama cha TANU kufanikiwa mbali na uwepo wa matatizo hayo?

A Kiliungwa mkono na mashujaa wengi wa kiafrika
B Kiliwaunganisha watu wa matabaka mbalimbali
C Kiliungana na vyama vingi vya siasa
D Wazungu wengi walikisaidia
E Viongozi wake walipendwa na wazungu

Mtahiniwa katika swali hili alitakiwa kubaini sababu zilizochangia chama cha TANU kufanikiwa katika harakati za kupigania uhuru mbali na uwepo wa matatizo yaliyoathiri vyama vingi vya siasa Afrika. Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa hafifu kwani ni watahiniwa 285,302 (25.8%) tu ndio waliweza kuchagua jibu sahihi *B, Kiliwaunganisha watu wa matabaka mbalimbali*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu harakati za ukombozi dhidi ya ukoloni Tanganyika. Vilevile, walikuwa na uelewa kuwa chama cha TANU kiliwaunganisha Watanganyika wote bila kujali uwezo wao wa kijamii, kiuchumi, rangi ya ngozi yao, dini na kabila ili kupata nguvu ya pamoja ya kudai uhuru.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 382,792 (34.6%) walichagua kipotoshi *A*, *Kiliungwa mkono na mashujaa wengi wa kiafrika.* Uchaguzi wa kipotoshi hiki unaonesha kuwa watahiniwa hao walikuwa na uelewa mdogo kuhusu harakati za ukombozi wa Tanganyika. Watahiniwa hao walipaswa kuelewa kuwa chama cha TANU kilitumia mbinu mbalimbali kujitangaza na kuwafikia watu nchi nzima. Kwa mfano, kutumia gazeti la Sauti ya Umma, lugha ya Kiswahili na michezo. Hivyo kuungwa mkono na mashujaa wengi wa Kiafrika haikuwa njia mojawapo ya kufikia mafanikio.

Aidha, jumla ya watahiniwa 316,492, (28.6%) walichagua kipotoshi *C*, *Kiliungana na vyama vingi vya siasa.* Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu harakati za kudai uhuru Tanganyika. Walipaswa kuelewa kuwa kila chama kilikuwa na falsafa na mbinu zake za kupigania uhuru, hivyo haikuwa rahisi kwa vyama hivyo

kuungana. Kwa mfano, chama cha United Tanganyika Party (UTP) kiliundwa baada ya kutofautiana kwa viongozi wa TANU.

Hali kadhalika, jumla ya watahiniwa 56,901 (5.1%) walichagua kipotoshi *D*, *Wazungu wengi walikisaidia.* Hilo halikuwa jibu sahihi kwani harakati za kudai uhuru wa Tanganyika ulikuwa dhidi ya wazungu (Waingereza). Hivyo, haikuwezekana na ni vigumu kwa wakoloni kuwasaidia watawaliwa kudai huru wao.

Vilevile, watahiniwa 52,498 (4.7%) walichagua kipotoshi *E*, *Viongozi wake walipendwa na wazungu.* Hilo halikuwa chaguo sahihi kwani wakati wa harakati za kudai uhuru, viongozi wengi walichukiwa na wakoloni kwa sababu walipinga unyonyaji. Kwa mfano Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, kiongozi wa TANU alishitakiwa na kutakiwa kulipa faini kwa kosa la kuwakosoa Wakuu wa Wilaya wawili.

**Swali la 24:** Mwalimu aliwafundisha wanafunzi wake sifa za sayari moja miongoni mwa sayari nane. Aliwaambia kuwa sayari hiyo ndiyo pekee yenye viumbe na robo tatu ya eneo lake ni maji. Je, sayari hiyo ni ipi?

A Kausi B Zuhura C Sumbula
D Mirihi E Dunia

**Jedwali Na. 13: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 63,297 | 79,590 | 73,116 | 52,633 | 823,314 | 15,849 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 5.7 | 7.2 | 6.6 | 4.8 | 74.3 | 1.4 |

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubaini sayari pekee yenye viumbe, na robo tatu ya eneo lake ni maji. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa ni wa kiwango kizuri kwani watahiniwa 823,314 (74.3%) walichagua jibu sahihi *E, Dunia*. Watahiniwa hao waliweza kubaini nafasi, sifa na mpangilio wa sayari katika mfumo wa Jua.

Kipotoshi *A, Kausi,* kilichaguliwa na watahiniwa 63,297 (5.7%); kipotoshi *B, Zuhura,* kilichaguliwa na watahiniwa 79.590 (7.2%); kipotoshi *C, Sumbula* kilichaguliwa na watahiniwa 73,116 (6.6%) *na* kipotoshi *D*, *Mirihi* kilichaguliwa na watahiniwa 52,633 (4.8%). Watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu sayari, sifa, mpangilio na nafasi za sayari katika mfumo wa Jua.

**Swali la 25:** Jika alisoma kitabu cha Darasa la Tatu na akagundua kuwa katika siku 365¼ au 366 hutokea vipindi tofauti ambavyo ni vuli, masika, kiangazi na kipupwe. Je, Jika alikuwa anasoma kuhusu nini?

A Dunia kujizungusha yenyewe
B Dunia kulizunguka jua
C Kupatwa kwa mwezi
D Kupatwa kwa jua
E Afelioni na perihelioni


Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubaini sababu ya kutokea kwa vipindi vya vuli, masika, kiangazi na kipupwe. Kwa ujumla ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani watahiniwa 528,804 (47.7%) walichagua jibu sahihi *B*, *Dunia kulizunguka Jua*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mizunguko ya Dunia na matokeo yake. Hivyo waliweza kutambua kuwa Dunia hutumia muda wa siku 365¼ hadi 366 kulizunguka Jua, na matokeo yake ni uwepo wa majira ya mwaka.

Watahiniwa 287,967 (26.0%) waliochagua kipotoshi *A*, *Dunia kujizungusha yenyewe kwenye muhimili wake* hawakuwa na maarifa kuhusu Dunia kulizunguka Jua na Dunia kujizungusha kwenye mhimili wake. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa mdogo kuhusu mizunguko ya Dunia na matokeo yake. Hivyo hawakuweza kubaini kuwa Dunia hutumia siku 365¼ au 366 kuzunguka Jua, na moja ya matokeo ya kitendo hiki ni kutokea kwa majira ya mwaka.

Vilevile, watahiniwa 94,058 (8.5%) walichagua kipotoshi *C*, *Kupatwa kwa mwezi* na watahiniwa 71,484 (6.5%) walichagua kipotoshi *D*, *Kupatwa kwa jua.* Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa kupatwa kwa Mwezi hutokea wakati Dunia inapopita katikati ya Jua na Mwezi na

kupatwa kwa Jua hutokea wakati Mwezi unapokuwa katikati ya Dunia na Jua. Kupatwa kwa Jua na Mwezi hutokea kwa kipindi kifupi sana kisichozidi dakika 10 hivyo hakuhusiani na majira ya mwaka.

Pia, watahiniwa 111,090 (10.0%) walichagua kipotoshi *E*, utofauti wa nafsi au umbali wa Dunia kutoka kwenye Jua. Watahiniwa hao walipaswa kuelewa kuwa, Perihelioni ni kipindi ambacho Dunia huwa karibu zaidi na Jua mwanzoni mwa mwezi wa Januari kila mwaka. Halikadhalika, Afelioni ni kipindi ambacho Dunia huwa mbali na Jua mwanzoni mwa mwezi Julai kila mwaka. Haya pia ni matokeo ya Dunia kulizunguka Jua. Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 25 umeoneshwa katika Chati Na. 9.




**Chati Na. 9**: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 25*

**Swali la 26:** Ikiwa umetakiwa na mwalimu wako wa Sayansi kueleza umuhimu wa kuota jua la asubuhi kwa wanafunzi wenzako ili kuimarisha afya; Je, ungewaeleza sababu ipi?

A Ni chanzo cha vitamini E
B Ni chanzo cha vitamini D
C Ni chanzo cha vitamini A
D Ni chanzo cha wanga
E Ni chanzo cha vitamin C

**Jedwali Na. 14: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 85,684 | 575,740 | 153,737 | 134,425 | 144,060 | 14,153 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 7.7 | 52.0 | 13.7 | 12.1 | 13.0 | 1.3 |

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubaini kwanini ni muhimu kiafya binadamu kuota Jua la asubuhi. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani watahiniwa 575,740 (52.0%) walichagua jibu sahihi *B*, *Ni chanzo cha vitamini D.* Watahiniwa hao walikuwa na uelewa kuhusu umuhimu wa vitamin D katika mwili wa binadamu. Kwa upande mwingine, watahiniwa 85,684 (7.7%) waliochagua kipotoshi *A*, *Ni chanzo cha vitamin E* hawakuelewa kuwa vitamin E, hupatikana kwa kula matunda kama mapapai, karoti na mboga za majani.

Vile vile, watahiniwa 153,737 (13.7%) walichagua kipotoshi *C, Ni chanzo cha vitamini A ;* watahiniwa 134,425 (12.1%) walichagua kipotoshi *D, Ni chanzo cha wanga;* na watahiniwa 138,781 (12.5%) walichagua kipotoshi *E, Ni chanzo cha vitamin C*. Watahiniwa hao hawakuwa na ufahamu kuhusu chanzo cha upatikanaji wa aina mbalimbali za vitamin. Vitamin A hupatikana kwa kula mboga za majani, vitamin D hupatikana kwa kula nafaka, na vitamin C hupatikana kwa kula matunda kama vile limao na machungwa.

**Swali la 27:** Mwalimu wa Maarifa ya Jamii alifanya mjadala wa jumla na wanafunzi wake kuhusu aina tatu za vipimio vya ramani. Je, vipimio vipi vya ramani walivijadili?


A Kidogo, uwiano na kati
B Kati, mstari na kikubwa
C Uwiano, sentensi na mstari
D Sentensi, kikubwa na mstari
E Kati, kidogo na kikubwa

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubaini aina tatu za kipimio cha ramani. Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa cha

wastani kwani watahiniwa 640,650 (57.8%) walichagua jibu sahihi *E, Kati, kidogo na kikubwa*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu kipimio cha ramani. Walifahamu kuwa kuna aina tatu za vipimio vya ramani.  Kipimio kidogo ambacho hutumika kuwakilisha maeneo makubwa kama nchi, bara na hata Dunia. Kipimio cha kati ambacho huwakilisha maeneo yenye ukubwa wa wastani kama wilaya na mkoa, na kipimio kikubwa kinachowakilisha maeneo madogo kama vile majengo, viwanja vya michezo na mashamba.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 100,290 (9.1%) walichagua kipotoshi *A*, *Uwiano, kidogo na kati.*  Watahiniwa hao walichanganya aina ya kipimio na njia ya kuwasilisha kipimio cha ramani. Watahiniwa wengine 75,458 (6.8%) waliochagua kipotoshi *B*, *Kati, mstari na kikubwa,* walikuwa na uelewa kuhusu kipimio. Hata hivyo walishindwa kubaini kuwa mstari ni njia inayotumika kuwasilisha kipimio cha ramani. Vile vile, watahiniwa 215,610 (19.5%) waliochagua kipotoshi *C*, *Uwiano, sentensi na mstari,* hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu kipimio cha ramani kwa kuwa vipengele hivi ni njia za kuwasilisha kipimio cha ramani.

Pia, watahiniwa 61,584 (5.6%) waliochagua kipotoshi *D*, *Sentensi, kikubwa na mstari,* hawakuwa na maarifa kuhusu kipimio kwa kuwa sentensi na mstari ni njia za kuwasilisha kipimio cha ramani. Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 27 umeoneshwa katika Chati Na. 10.




**Chati Na. 10**: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 27*

**Swali la 28:** Bwana Pazi kutoka Gitega 30$^o$ Mashariki alitaka kujua tofauti ya muda kati ya nchi yake na Accra ambako rafiki yake Kiko huishi. Ni mistari ipi ya kufikirika ungemshauri atumie ili kupata tofauti ya muda baina ya miji hiyo?

A Latitudo
B Tropiki ya Kansa
C Longitudo
D Ikweta
E Tropiki ya Kaprikoni

**Jedwali Na. 15: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 210,127 | 124,281 | 448,705 | 230,034 | 80,792 | 13,860 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 19.0 | 11.2 | 40.5 | 20.8 | 7.3 | 1.3 |

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kutambua mstari wa kufikirika unaotumika kutafuta tofauti ya muda baina ya miji. Kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 448,705 (40.5%) walichagua jibu sahihi *C*, *Longitudo*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa kuhusu maana na kazi za mistari mbalimbali inayochorwa kwenye ramani (mahali, nafasi na kukukotoa muda). Hata hivyo, watahiniwa 7,987 (0.7%) waliochagua kipotoshi *A*, *Latitudo,* walishidwa kutofautisha kazi za longitudo na latitudo.

Watahiniwa wengine 124,281 (11.2%) walichagua kipotoshi *B*, *Tropiki ya Kansa;* watahiniwa 230,034 (20.8%) walichagua kipotoshi *D*, *Ikweta;* na watahiniwa 80,792 (7.3%) walichagua kipotoshi *E*, *Tropiki ya Kaprikoni.* Watahiniwa hao hawakuwa na uelewa kuhusu majina na kazi mbalimbali za mistari ya kufikirika inayotumika kwenye ramani.

**Swali la 29:** Ni neno lipi zuri linaloweza kutumika kumwelezea mtu mwenye uwezo binafsi katika kubadili mawazo na kuyaweka kwenye vitendo?

A Mwekezaji B Mjasiriamali C Msanii
D Msanifu E Mwajibikaji

Katika kujibu swali hili, mtahiniwa alitakiwa kubaini neno linaloweza kutumika kumwelezea mtu mwenye uwezo binafsi katika kubadili mawazo na kuyaweka kwenye vitendo. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa hafifu kwani watahiniwa 395,758 (35.7%) walichagua jibu sahihi *B*, *Mjasiriamali*. Watahiniwa hao walioweza kubaini jibu sahihi, walikuwa na maarifa ya kutosha kuwa mjasiriamali ni mtu anayefanya biashara kwa kufanya ubunifu, utafutaji wa fedha na kujishughulisha katika kutafuta faida.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 112,668 (10.2%) waliochagua kipotoshi *A*, *Mwekezaji* walikuwa na maarifa kuhusu ujasiriamali, lakini walishindwa kubaini kuwa mwekezaji ni mtu mwenye mtaji mkubwa wa fedha au teknolojia. Mwekezaji hutumia fedha hiyo kuwekeza katika biashara fulani ili aweze kupata faida.

Watahiniwa wengine 205,048 (18.5%) walichagua kipotoshi *C*, *Msanii.* Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa kuwa msanii ni mtu anayetumia kipaji chake katika kuelimisha na kuburudisha jamii. Watahiniwa walisukumwa kuchagua kipotoshi hiki kwa kuwa msanii pia hutumia ubunifu katika kazi zake za sanaa. Pia, kwa hivi sasa wapo wasanii wengi waliojipatia fedha nyingi hivyo kufirikiri kuwa usanii ni sawa na biashara.

Watahiniwa 166,113 (15.0%) waliochagua kipotoshi *D*, *Msanifu,* walikuwa na maarifa kuwa ni mtu anayetumia kipaji chake kubuni kazi za sanaa kwa lengo la kujipatia kipato. Watahiniwa walisukumwa kuchagua kipotoshi hiki kwa kuwa pia msanifu hutumia ubunifu katika kazi zake za sanaa. Hata hivyo, halikuwa jibu sahihi.

Vilevile, watahiniwa 214,144 (19.3%) waliochagua kipotoshi *E*, *Mwajibikaji,* hawakuwa na maarifa kuwa huyu ni mtu anayetimiza

majukumu yake kwa wakati bila shinikizo, na sio mtu anayebadilisha wazo na kulikweka katika hali ya vitendo. Watahiniwa hao walihusianisha na mazingira wanayoishi kwa kuwa wanaona jinsi wajasiriamali wanavyojituma.

**Swali la 30:** Katika ujasiriamali, neno uthubutu linamaanisha nini?

A Kuwa na maamuzi magumu
B Uzembe katika kufanya maamuzi
C Kuwa tayari kujitolea
D Kusababisha hasara kwa makusudi
E Kuwa jasiri kuchukua hatua

**Jedwali Na. 16: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 201,800 | 115,929 | 292,115 | 118,516 | 362,696 | 16,743 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 18.2 | 10.5 | 26.4 | 10.7 | 32.7 | 1.5 |

Mtahiniwa kwenye swali hili alitakiwa kubaini maana ya neno *uthubutu* katika ujasiriamali. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa hafifu kwani watahiniwa 362,696 (32.7%) walichagua jibu sahihi *E, Kuwa jasiri kuchukua hatua*. Watahiniwa hao walioweza kubaini jibu sahihi walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu ujasiriamali, umuhimu wake na ubora wa mjasiriamali mzuri.

Hata hivyo, watahiniwa 201,800 (18.2%) waliochagua kipotoshi *A, Kuwa na maamuzi magumu,* hawakuwa na maarifa kuhusu sifa za mjasiriamali, kwa kuwa maamuzi magumu yanaweza yakasababisha hasara katika biashara. Watahiniwa 115,929 (10.5%) waliochagua kipotoshi *B, Uzembe katika kufanya maamuzi*, hawakuwa na maarifa kuhusu sifa za mjasiriamali kwa kuwa kitendo hicho husababisha kuchelewa kufikia malengo.

Vilevile, watahiniwa 292,115 (26.4%) waliochagua kipotoshi *C*, *Kuwa tayari kujitolea,* hawakuwa na uelewa kuwa dhana hii ya utayari wa kufanya jambo bila malipo yoyote haliendani na ujasiriamali. Kwani ni lazima ujasiriamali uoneshe tija, hivyo si sahihi

kuwa jambo hili ni sawa na uthubutu. Kipotoshi *D, Kusababisha hasara kwa makusudi,* kilichaguliwa na watahiniwa 118,516 (10.7%). Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa yoyote, kwani hakuna uhusiano wowote uliopo kati ya neno uthubutu na kusababisha hasara kubwa, hivyo walijibu kwa kubuni tu.

**Swali la 31:** Mjasiriamali anatakiwa kuwa mbunifu ili bidhaa au huduma yake iweze kununuliwa. Je, atafanya nini ili kuwashawishi wateja?

A Ataacha kufanya biashara
B Atawalazimisha wateja kununua
C Atawaelekeza maduka ya jirani
D Ataongeza ukubwa wa biashara
E Atawapa wateja zawadi

Swali lilimtaka mtahiniwa kubaini mbinu atakazotumia mjasiriamali kuwashawishi wateja kununua bidhaa. Jibu sahihi lilikuwa *E, Kuwapa wateja zawadi*. Jumla ya watahiniwa 244,036 (22.0%) walioweza kubaini jibu sahihi walikuwa na uelewa wa njia nzuri kulingana na swali waliloulizwa. Kwa upande mwingine, watahiniwa 43,367 (3.9%) waliochagua kipotoshi *A, Kuacha kufanya biashara* hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu ujasiriamali kwa kuwa jibu hilo sio mbinu sahihi ya kuwavutia wateja katika biashara.

Jumla ya watahiniwa 90,767 (8.2%) waliovutiwa na kipotoshi *B, Atawalazimisha wateja kununua bidhaa,* hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu ujasiriamali, kwa kuwa hii sio njia sahihi ya kuendesha biashara. Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa kuwalazimisha wateja kununua bidhaa itawafanya wakimbie biashara yako.

Vilevile, watahiniwa 82,945 (7.7%) waliochagua kipotoshi *C, Atawaelekeza maduka ya jirani,* walikuwa na maarifa kuwa hali hiyo utokea katika jamii. Pale mteja anapokosa bidhaa katika duka fulani huelekezwa kwenda kwenye duka ambalo anaweza kupata bidhaa hiyo. Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa kitendo hicho huchangia kupoteza wateja, na sio kuwavutia.

Pia, watahiniwa 134,425 (12.0%) waliochagua kipotoshi *D, Ataongeza ukubwa wa biashara,* walikuwa na maarifa kuhusu ujasiriamali. Aidha, walishindwa kuelewa ukweli kwamba kupanua biashara tu sio kigezo muhimu cha kuvutia wateja.

**Swali la 32:** Wanafunzi wa Darasa la Saba walitembelea shamba kubwa la ufugaji wa mbuzi wa kisasa. Je, hiyo ni aina gani ya ufugaji?

A Ufugaji wa jadi
B Ranchi
C Ufugaji wa ndani
D Ufugaji wa kuhamahama
E Ufugaji wa sehemu moja

Swali lilimtaka mtahiniwa kutambua aina ya ufugaji unaofanyika katika mashamba makubwa. Jumla ya watahiniwa 319,967 (28.9%) walichagua jibu sahihi *B*, *Ranchi*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa kuhusu njia mbalimbali za ufugaji wa wanyama. Watahiniwa 114,906 (10.4%) walivutiwa kipotoshi *A, Ufugaji wa jadi*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa kuhusu ufugaji, lakini walishindwa kuelewa maana ya ufugaji wa jadi. Ufugaji wa jadi ni wa kupeleka mifugo malishoni asubuhi na kuwarudisha zizini wakati wa jioni.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 328,046 (29.6%) waliovutiwa na kipotoshi *C, Ufugaji wa ndani*, walikuwa na maarifa kuhusu ufugaji, Aidha, walishindwa kuelewa kuwa ufugaji wa ndani ni ule unaofanyika katika eneo la kudumu (ndani), na si lazima liwe ni eneo kubwa. Vilevile, watahiniwa 69,036 (6.2%) walivutiwa na kipotoshi *D, ufugaji wa kuhamahama*. Watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa ufugaji wa kuhamahama ni ule wa kuhamahama na mifugo kutafuta malisho na maji. Kwa mfano, ufugaji wa kuhamahama hufanywa na jamii ya Wamasai na Wasukuma nchini Tanzania.

Pia watahiniwa 260,631 (23.5) waliovutiwa na kipotoshi *E, Ufugaji wa sehemu moja,* hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu ufugaji. Watahiniwa hao walipaswa kuelewa kuwa kwenye ufugaji wa sehemu moja, mifugo hufugwa na kulishwa katika eneo

ililozungushiwa uzio, hivyo humruhusu mfugaji kufuga mifugo michache.

**Swali la 33:** Kukua kwa sekta ya viwanda na usafirishaji nchini Tanzania ni matokeo ya kuimarika kwa shughuli mama ya kiuchumi. Ipi kati ya zifuatazo ina sifa ya kuitwa shughuli mama ya kiuchumi?

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| A | Utalii | B | Ufugaji | C | Uchimbaji madini |
| D | Misitu | E | Kilimo | | |

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubaini shughuli mama ya kiuchumi Tanzania, ambayo ni kichocheo cha ukuaji wa sekta ya viwanda. Jumla ya watahiniwa 655,322 (59.2%) walichagua jibu sahihi *E, Kilimo*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuwa kilimo ni shughuli ya uzalishaji mali iliyoajiri watu wengi kuliko shughuli nyingine yoyote nchini Tanzania. Inakadiriwa kuwa asilimia 65.5 ya Watanzania wameajiriwa katika shughuli za kilimo.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 175,795 (15.9%) waliochagua kipotoshi *A Utalii,* hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu shughuli mama ya kiuchumi nchini Tanzania. Watahiniwa hao walipaswa kujua utalii sio shughuli mama ya kiuchumi kwa kuwa imeajiri watu wachache nchini Tanzania. Hata hivyo, watahiniwa 94,440 (8.5%) waliochagua kipotoshi *B, Ufugaji,* walishindwa kuelewa kuwa ufugaji sio shughuli mama ya kiuchumi nchini Tanzania.

Vilevile, watahiniwa 223,800 (10.3%) waliochagua kipotoshi *C, Uchimbaji wa madini,* hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu shughuli mama ya kiuchumi Tanzania. Watahiniwa hao walipaswa kuelewa kuwa uchimbaji madini hutoa ajira kwa Watanzania wachache, hivyo hukosa sifa ya kuwa shughuli mama ya kiuchumi Tanzania.

Pia, watahiniwa 53,846 (4.9%) waliochagua kipotoshi *D, Misitu,* hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu shughuli mama za kiuchumi nchini Tanzania. Watahiniwa hao walipaswa kuelewa kuwa, shughuli mama ya kiuchumi ni ile inayoajiri watu wengi. Misitu

huajiri watanzania wachache, hivyo hukosa sifa ya kuwa shughuli mama ya kiuchumi Tanzania.

**Swali la 34:** Kitu gani kinaweza kuchangia kukua kwa uzalishaji mali nchini Tanzania?

A Uwepo wa mifumo rafiki ya kisera na kisheria
B Uwepo wa viwanda vingi nchini
C Kukaribisha wawekezaji kutoka nje ya nchi
D Kuwa na amani na utulivu mijini
E Kutangaza vivutio vyetu Ulaya

**Jedwali Na. 17: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 220,028 | 423,343 | 234,732 | 119,558 | 95,016 | 15,122 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 19.9 | 38.2 | 21.2 | 10.8 | 8.6 | 1.4 |

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubaini jambo linalochangia kukuwa kwa uzalishaji mali nchini Tanzania. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa hafifu kwani watahiniwa 220,028 (19.9%) waliweza kuandika jibu sahihi *A, Uwepo wa mifumo rafiki ya kisera na kisheria*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuwa sera nzuri zinazovutia uzalishaji mali na sheria rafiki zinazolenga kulinda wazalishaji mali, huchangia kukua kwa uzalishaji mali nchini.

Jumla ya watahiniwa 423,343 (38.2%) waliochagua kipotoshi *B, Uwepo wa viwanda vingi,* walikuwa na maarifa kuwa uzalishaji kupitia viwanda unapokuwa mkubwa tunaweza kupata fedha za kutosha. Watahiniwa hao hawakutambua kuwa uwepo wa viwanda bila mifumo rafiki ya kisera na kisheria, viwanda haviwezi kufanya kazi ipasavyo, na mwishowe kushindwa kabisa kuzalisha bidhaa.

Kipotoshi *C, Kukaribisha wawekezaji kutoka nje,* kilichaguliwa na watahiniwa 234,732 (21.2%). Watahiniwa hao walikuwa na maarifa kuwa uwepo wa wawekezaji utalipatia taifa fedha kupitia ulipaji wa kodi na ruzuku. Hata hivyo, walishindwa kutambua kuwa bila ya

uwepo wa sera na sheria rafiki, wawekezaji hawawezi kuwekeza hapa nchini.

Vilevile, watahiniwa 119,558 (10.8%) waliochagua kipotoshi *D, Kuwa na amani na utulivu mijini,* walikuwa na maarifa kuwa hali hiyo ndiyo itakayowawezesha watu kufanya kazi. Hata hivyo, watahiniwa hao hawakuelewa kuwa amani na utulivu pekee havichangii kukua kwa uzalishaji mali. Watahiniwa walijibu kwa kuhusianisha na taarifa nyingi zinazosisitiza amani kama kichocheo muhimu cha maendeleo.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 192,675 (17.4%) walichagua kipotoshi *E, Kutangaza vivutio vyetu Ulaya.* Watahiniwa hao walihusisha uwepo wa vivutio vingi vya utalii nchini na ukuaji wa shughuli za uzalishaji mali. Hii ina maana kuwa, kufahamika kwa vivutio hivyo kutaongeza watalii jambo ambalo ni sahihi. Lakini, walishindwa kubaini kuwa hata utalii unahitaji uwepo wa mikakati madhubuti ili kuweza kujiendesha kwa ufanisi.

**Swali la 35:** Bahati na Asia wanamiliki kiwanda cha kutengeneza mikate chenye wafanyakazi sabini na mtaji wa milioni mia tano. Je, huu ni ujasiriamali wa kundi gani?

A Ujasiriamali biashara mdogo mdogo
B Ujasiriamali biashara mdogo
C Ujasiriamali biashara mkubwa
D Ujasiriamali biashara mkubwa zaidi
E Ujasiriamali biashara wa kati

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubaini kundi la ujasiriamali linalomiliki wafanyakazi sabini na mtaji wa milioni mia tano. Ufaulu katika swali hili ulikuwa hafifu kwani watahiniwa 192,675 (17.4%) tu ndio walichagua jibu sahihi *E, Ujasiriamali biashara wa kati*. Watahiniwa walioweza kubaini jibu sahihi walikuwa na maarifa ya kutosha kuwa hili ni kundi lenye wafanyakazi kati ya 50 hadi 99, na mtaji wa zaidi ya milioni mia mbili hadi milioni mia nane.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 132,416 (12%) walichagua kipotoshi *A, Ujasiriamali biashara mdogo mdogo.* Watahiniwa hao walikuwa na maarifa kuhusu makundi ya ujasiriamali. Lakini walishindwa kutambua kuwa kundi hili lina wafanyakazi wasiozidi 4 na mtaji wa milioni 5.

Kipotoshi *B, Ujasiriamali biashara mdogo,* kilichaguliwa na watahiniwa 89,387 (8.1%). Watahiniwa hao hawakutambua kuwa kundi hili lina wafanyakazi 5 hadi 49, na mtaji wa kuanzia milioni 5 hadi milioni 200. Watahiniwa walijibu kutokana na mazoea ya wajasiriamali wadogo wadogo wanaopatikana katika mazingira yao.

Vile vile 445,807 (40.2%) walichagua kipotoshi *C, Ujasiriamali biashara mkubwa.* Watahiniwa hao walishindwa kutambua kuwa kundi hili lina wafanyakazi 100 na zaidi, na mtaji wake ni milioni 800. Pia, watahiniwa 233,485 (21.1%) waliochagua kipotoshi *D, Ujasiriamali biashara mkubwa zaidi,* hawakutambua kuwa hakuna kundi kama hili katika ujasiriamali.

**Swali la 36:** Katika kipindi cha Stadi za Kazi wanafunzi walijifunza vitu mbalimbali vitumikavyo wakati wa kuigiza. Je, mavazi avaayo mwigizaji wakati wa kuigiza huitwaje?

A Koti B Zana C Mapambo
D Maleba E Gauni


Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubaini jina la mavazi avaayo mwigizaji wakati wa kuigiza. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani watahiniwa 635,040 (57.3%) walichagua jibu sahihi *D*, *Maleba.* Watahiniwa hao walioweza kubaini jibu sahihi walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mavazi yanayovaliwa na waigizaji.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 45,470 (4.1%) walichagua kipotoshi A*, Koti.* Uchaguzi wa kipotoshi hiki unatokana na uzoefu walionao kwani michezo mingi ya kuigiza inayoonekana katika runinga imetawaliwa na vazi la koti. Hivyo, kufikiri kuwa hili ni vazi maalumu kwa ajili ya waigizaji. Vile vile, watahiniwa 162,911 (14.7%) walichagua kipotoshi *B, Zana.* Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa kuhusu mavazi kwa kuwa zana ni vifaa vyovyote

vinavyotumika katika igizo. Watahiniwa hao walijibu kwa kuzingatia mazingira yao ya kawaida kwamba kila kazi huhitaji vifaa ili kuifanya kwa weledi.

Hali kadhalika, watahiniwa 203,844 (18.4%) walichagua kipotoshi *C, Mapambo.* Uchaguzi wa kipotoshi hiki unaonesha kuwa walikuwa na maarifa kuhusu uigizaji kuwa huhitaji mapambo. Hata hivyo, walishindwa kutambua kuwa hata hayo mapambo yanapovaliwa na mwigizaji huwa sehemu ya maleba.

Kipotoshi *E, Gauni* kilichaguliwa na watahiniwa 46,439 (4.2%). Watahiniwa hao walishindwa kutambua kwamba nguo hii huvaliwa na wanawake katika mazingira ya kawaida na siyo nguo rasmi inayovaliwa na waigizaji wakati wa kuigiza. Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 36 umeoneshwa katika Chati Na. 11.




**Chati Na. 11**: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 36*

**Swali la 37:** Katika biashara, wapo wajasilimali ambao wanafanya udanganyifu ili kujiongezea kipato. Ni kwa namna gani wajasiliamali hufanya udanganyifu?

A Kuongeza thamani ya bidhaa
B Kutotambua mahitaji yao
C Kuwazidishia wateja chenji
D Kuchezea vipimo
E Kutolipa kodi kwa wakati

**Jedwali Na. 18: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 409,536 | 111,632 | 85,873 | 278,036 | 207,399 | 15,323 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 37.0 | 10.1 | 7.8 | 25.1 | 18.7 | 1.4 |

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubaini namna ambavyo wajasiriamali hufanya udanganyifu katika biashara ili kujiongezea kipato. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa hafifu kwani ni watahiniwa 278,036 (25.1%) tu ndio walichagua jibu sahihi *D, Kuchezea vipimo*. Watahiniwa hao walibaini kuwa udanganyifu hufanyika kwa kuchezea vipimo hivyo kutotoa vipimo sahihi. Kutokana na hali hiyo, wateja hupunjwa bidhaa na wajasiriamali kupata faida kubwa. Watahiniwa pia wana maarifa kuwa katika vipimo visivyo rasmi, wajasiriamali huponda makopo ya kupimia bidhaa kama mkaa na viazi kwa lengo la kupunguza ujazo wa bidhaa, huku malipo yakibakia kuwa ya kawaida. Hali hii pia huwapa wajasiriamali faida kubwa na kujiongezea kipato.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 409,536 (37.0%) walichagua kipotoshi *A, Kuongeza thamani ya bidhaa.* Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa kitendo hiki huongeza thamani ya bidhaa, hivyo wateja kuvutiwa na kuwa tayari kununua. Hivyo, huu si udanganyifu bali ni ubunifu wa kukuza biashara na kuvutia wateja. Vilevile, watahiniwa 111,632 (10.1%) waliochagua kipotoshi *B, Kutotambua mahitaji yao,* hawakuwa na maarifa ya kutosha kwa kuwa hali hii huwafanya wajasiriamali kutopata wateja, jambo linalowasababishia kupata hasara.

Jumla ya watahiniwa 85,873 (7.8%) walichagua kipotoshi *C, Kuwazidishia wateja chenji.* Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kwa kuwa kitendo hicho hakimpi mjasiriamali faida bali hasara. Kumzidishia mteja chenji maana yake ni kutoa sehemu ya faida au mtaji kumwongezea mteja bila kujua.

Pia watahiniwa 207,399 (18.7%) waliochagua kipotoshi *E, Kutolipa kodi kwa wakati,* hawakuwa na maarifa kuwa kitendo hicho

kinaweza kusababisha biashara kufungwa au kufilisiwa pindi mamlaka za kukusanya kodi watakapobaini. Watahiniwa walihusianisha na hali halisi ya mazingira wanayoishi ambapo wajasiriamali huzungumzia vitendo vya kutokulipa kodi kwamba vinawafanya wapate faida kubwa.


**Swali la 38:** Mwalimu aliwaagiza wanafunzi wa Darasa la Tano kuandaa na kufungasha chakula kwa matumizi yao wakati wa ziara ya kimasomo. Ni chakula kipi walipaswa kuandaa?

A Wali na maharage
B Ugali na maharage
C Ndizi na nyama ya mchuzi
D Ndizi na nyama za kubanika
E Wali na mchuzi wa samaki

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubaini chakula ambacho kinafaa kufungashwa kwa ajili ya ziara ya kimasomo. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani kwani watahiniwa 619,210 (55.9%) walichagua jibu sahihi *D*, Ndizi *na nyama za kubanika.* Watahiniwa hao walibaini kuwa ili vyakula vidumu kwa muda mrefu bila kuharibika ni lazima vipunguzwe maji. Hivyo walitambua kuwa kubanika ni njia sahihi kupunguza kiwango cha maji katika vyakula.

Jumla ya watahiniwa 225,643 (20.4%) walichagua kipotoshi *A, Wali na maharage.* Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu namna ya kuandaa vyakula vya safari. Walihusianisha na mazingira ya jamii zao kwa kuwa hivyo ni miongoni mwa vyakula maarufu na vinapendwa na walio wengi. Lakini, hawakutambua kuwa maji yanayopatikana katika vyakula hivyo, huvifanya viharibike kwa urahisi na mapema. Vilevile, watahiniwa 115,980 (10.5%) waliochagua kipotoshi *B*, *Ugali na maharage* walihusianisha mazingira ya shuleni na nyumbani. Hii ni kwa kuwa vyakula hivi ni miongoni mwa vyakula maarufu, lakini walishindwa kutambua kuwa havifai kubeba safarini.
Pia, watahiniwa 70,194 (6.3%) walichagua kipotoshi *C*, *Ndizi na nyama ya mchuzi,* na watahiniwa 61,940 (5.6%) walichagua kipotoshi *E*, *Wali na mchuzi*. Watahiniwa hao walitakiwa kujua kuwa

swali liliwataka kutaja vyakula wanavyoweza kuandaa wenyewe na kuvitumia wakiwa safarini. Vyakula hivyo havitakiwi kuwa vya majimaji, kwani aina hiyo huharibika haraka. Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 38 umeoneshwa katika Chati Na. 12.




**Chati Na. 12**: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 38*

**Swali la 39:** Viatu ni sehemu ya sare za shule. Kwa nini wanafunzi wanashauriwa kutovaa viatu vyenye visigino virefu?

A Husababisha maumivu ya tumbo
B Husababisha maumivu ya magoti
C Husababisha maumivu ya kichwa
D Husababisha maumivu ya misuli
E Husababisha maumivu ya kifua

**Jedwali Na. 19: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 45,277 | 268,162 | 50,321 | 701,151 | 29,399 | 13,489 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 4.1 | 24.2 | 4.5 | 63.3 | 2.7 | 1.2 |

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubaini sababu inayofanya washauriwe kutovaa viatu vyenye visigino virefu. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa kiwango kizuri kwani watahiniwa 701,151 (63.3%) waliweza kuchagua jibu sahihi *D*, *Husababisha maumivu ya*

*misuli*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuwa viatu virefu husababisha misuli kujivuta, hivyo kusababisha maumivu ya misuli, miguu na mgongo. Kwa upande mwingine, watahiniwa 45,277 (4.1%) waliochagua kipotoshi A, *Husababisha maumivu ya tumbo,* hawakuwa na maarifa ya kutosha kuwa jambo hilo halina uhusiano na maumivu ya misuli.

Vilevile, watahiniwa 268,162 (24.2%) waliochagua kipotoshi *B, Husababisha maumivu ya magoti;* 50,321 (4.5%) walichagua *C*, *Husababisha maumivu ya kichwa;* na 29,399 (2.7%) waliochagua *E*, *Husababisha maumivu ya kifua;* hawakuwa na maarifa ya kutosha kwa kuwa walishindwa kutambua kuwa maumivu ya misuli ya miguu hayana uhusiano na maumivu ya kichwa wala kifua.

**Swali la 40:** Wakati wa somo la Stadi za Kazi mwalimu aliwaambia wanafunzi kuwa, haitakiwi kukamua sweta kama sehemu ya kutoa maji baada ya kufua. Kwanini mwalimu alitoa tahadhari hiyo?


A Ili kuzuia kuchanika kwa sweta
B Kuepuka kuharibu nyuzi za sweta
C Ili kutokuharibu rangi ya sweta
D Kuepusha sweta kupata ukungu
E Kutokuharibu mwonekano wa sweta

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubaini tahadhari ya kutokukamua sweta baada ya kufua. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa hafifu kwani jumla ya watahiniwa 182,604 (16.5%) walichagua jibu sahihi *E, Kutoharibu mwonekano wa sweta*. Watahiniwa hao walikuwa na ufahamu wa namna ya kufua nguo za aina mbalimbali. Hivyo, waliweza kutambua kuwa ukamuaji wa nguo za aina hii huchangia kuongezeka ukubwa kwenye mikono, mabega na maeneo ya shingo.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 114,050 (10.3%) walichagua kipotoshi *A, Ili kuzuia kuchanika kwa sweta,* walihusianisha na mazingira yao ya nyumbani ambapo wanapofua na kukamua sweta, husikia likitoa mlio wa nyuzi kukatika.

Vilevile, watahiniwa 444,414 (40.1%) waliochagua kipotoshi *B*, *Kuepuka kuharibu nyuzi za sweta,* walikuwa na maarifa kuwa nguo ya aina hii ina tabia ya kuvutika nyuzi. Pia, watahiniwa 260,068 (23.5%) waliovutiwa na kipotoshi *C*, *Ili kutoharibu rangi ya sweta* walihusianisha na mazingira yao ambapo wanapofua sweta huona maji yakibadilika rangi na kufanana na rangi ya sweta. Lakini walishindwa kutambua kuwa majibu yote haya huchangia kuharibika kwa mwonekano wa sweta.

Watahiniwa wengine 91,069 (8.2%) waliochagua kipotoshi *D*, *Kuepuka sweta kupata ukungu,* hawakuwa na maarifa kuwa ukungu wa nguo husababishwa na nguo kuwekwa kwenye unyevu kwa muda mrefu. Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 40 umeoneshwa katika Chati Na. 13.





**Chati Na. 13**: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 40*

## 2.2 Sehemu B: Maswali ya Majibu Mafupi

**Swali la 41:** Ni madhara yapi mawili husababishwa na kilimo kisichofaa kwenye miteremko ya milima?

Swali hili lilimpima mtahiniwa uwezo wa kubaini madhara yanayosababishwa na kilimo kisichofaa kwenye miteremko ya milima. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani jumla ya watahiniwa 115,636 (10.4%) walipata alama zote 02,


watahiniwa 484,964 (43.8%) walipata alama 01, na watahiniwa 507,199 (45.8%) walipata 0. Chati Na. 14 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 41.




**Chati Na. 14**: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 41*

Watahiniwa 115,636 (10.4) waliopata alama 02 waliweza kuandika majibu mawili yaliyotakiwa ambayo ni kati ya haya: *mmomonyoko wa udongo na ardhi kupoteza rutuba*. Watahiniwa hawa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu athari za kilimo kisichofaa kwenye miteremko.

Watahiniwa 484,964 (43.8%) waliandika jibu moja sahihi. Watahiniwa hawa walikuwa na maarifa ya wastani kuhusu athari za kilimo kisichofaa. Kielelezo Na. 1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa mwenye ujuzi na maarifa ya kutosha.





**Kielelezo Na. 1:** *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 41*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 507,119 (45.8%) walipata 0 katika swali hili. Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa kuhusu athari za kilimo kisichofaa, hivyo walishindwa kutaja athari yoyote. Badala yake waliandika majibu kama; *Mazao kushindwa kuota, kuharibu vyanzo vya maji na ukame*. Vilevile, watahiniwa wengine

waliandika mlipuko wa volkano; hawa walihusianisha na majanga ya asili yanayotokea katika Dunia.

Kwa ujumla, watahiniwa hao walihusianisha athari za kilimo kwenye miteremko ya milima, na athari za mabadiliko ya tabia nchi. Baadhi ya watahiniwa hawakujibu chochote, hii ilidhihirisha kutokuwa na maarifa yoyote juu madhara ya kilimo kisichofaa kwenye miteremko ya milima. Kielelezo Na. 2 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa.


SWALI LA 41


i) Mafuriko

ii) Maporomoko ya ardhi

**Kielelezo Na. 2**: *Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 41*


**Swali la 42:** Carl Peters na Chifu Mangungo wa Msovero, Morogoro walisaini mkataba wa ulaghai. Je, mkataba huo ulihusu nini?

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kueleza maudhui ya mkataba wa ulaghai kati ya Carl Peters na Chifu Mangungo wa Msovero, Morogoro. Kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa ni hafifu kwani watahiniwa wengi 980,580 (88.5%) walipata sifuri. Watahiniwa katika kategoria hii walionesha ukosefu wa maarifa kuhusu uhusiano wa Tanzania na nchi za Ulaya kabla ya ukoloni. Watahiniwa hao walitaja majibu yasiyosahihi kama vile; Mkataba wa Heligoland, Mkutano wa Berlin na Mkataba wa ulaghai. Majibu haya yasiyo sahihi yanaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu vitangulizi vya mwanzo vya ukoloni na kazi walizofanya katika kuwaanda Waafrika kukubali ukoloni na kuitawala Tanganyika. Kielelezo Na. 3 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa.


SWALI LA 42 biashara ya Utumwa

**Kielelezo Na. 3:** *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 42*

Pamoja na hayo, ni watahiniwa 127,219 (11.5%) tu ndio walioweza kupata alama 2. Watahiniwa hao waliweza kuelezea maudhui ya mkataba huo wa kilaghai, na wenye kutia mashaka uliosainiwa kati ya Carl Peters na chifu Mangungo wa Msovero, Morogoro. Watahiniwa hao waliweza kueleza kwamba kupitia mkataba huo Mangungo alikabidhi sehemu kubwa ya ardhi/himaya yake kwa Carl Peters. Vilevile, watahiniwa hao walikuwa na uelewa kwamba machifu wa Kiafrika kama vile Mangungo hawakujua lugha ya kigeni hivyo hakuelewa hila na ubaya wa mikataba hiyo na alikubali. Kielelezo Na. 4 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa mwenye ujuzi na maarifa ya kutosha.



SWALI LA 42
Carl peters alimdanganya chifu mangungo ili asaini hule mkataba ili kuutwaa la ardhi yake

**Kielelezo Na. 4:** *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 42*

**Swali la 43:** Wanafunzi wa Darasa la Sita katika Shule ya Msingi Mwenge wanapanga safari ya kimasomo kwenda katika eneo la Engaruka lililopo Kaskazini mwa Tanzania. Ni masalia gani ya kihistoria watayaona katika eneo hilo?

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubaini masalia ya kihistoria ambayo wanafunzi wataona katika eneo la kihistoria la Engaruka. Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa hafifu kwani watahiniwa wengi 935,270 (84.4%) walipata sifuri. Watahiniwa katika kategoria hii walionesha ukosefu wa maarifa kwenye umahiri uliyotahiniwa. Baadhi ya majibu yasiyo sahihi yaliyotolewa na watahiniwa hao ni pamoja *Mabaki ya watu wa kale, Fuvu la mtu wa kale, Michoro ya mapangoni na Masalia ya zana za Mawe za Mwanzo*. Majibu haya yasiyo sahihi yanaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na uelewa kuhusu utunzaji wa kumbukumbu za matukio


ya kihistoria. Kielelezo Na. 5 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa.


SWALI LA 43

masalia ya zama za mawe za Kale.

**Kielelezo Na. 5:** *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 43*


Pamoja na hayo, ni watahiniwa 172,529 (15.6%) tu ndio walioweza kupata alama zote 2. Watahiniwa hao waliweza kueleza kwa ufasaha matukio la kihistoria yanayopatikana katika eneo la Engaruka. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa kuwa eneo hili ni maarufu kwa kuwa na mabaki ya masalia ya chuma na mifumo ya kilimo cha umwagiliaji iliyotumika na watu wa kale katika eneo hilo. Kielelezo Na. 6 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa mwenye ujuzi na maarifa ya kutosha.


SWALI LA 43 Masalia ya Vifaa Vya Kilimo Cha Umwagiliaji

**Kielelezo Na. 6:** *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 43*

**Swali la 44:** Mabadiliko ya tabianchi yamekuwa yakiathiri sekta ya kilimo. Bainisha athari mbili za tabianchi katika kilimo.


Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubainisha athari mbili za tabianchi katika kilimo. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa hafifu kwani watahiniwa 89,651 (8.1%) walipata alama zote 02, watahiniwa 246,524 (22.3%) walipata alama 01, na watahiniwa 771,624 (69.7%) walipata 0. Chati Na. 15 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 44.




**Chati Na. 15**: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 44*

Katika kujibu swali hili, watahiniwa 89,651 (8.1%) walipata alama 02 kwa kuwa waliandika majibu sahihi mawili. Baadhi ya watahiniwa waliandika vipindi virefu vya ukame na mvua zisizotabirika, na mabadiliko ya misimu na ongezeko la wadudu waharibifu wa mazao. Hii inadhihirisha kuwa watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu athari za mabadiliko ya tabianchi katika kilimo.


Watahiniwa 246,524 (22.3%) walipata alama 01 kwa kuwa waliandika jibu moja sahihi, na lingine lisilo sahihi, au waliandika jibu moja tu sahihi. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa kiasi kidogo kuhusu athari za mabadilko ya tabianchi katika kilimo. Kielelezo Na. 7 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa mwenye ujuzi na maarifa ya kutosha.




**Kielelezo Na. 7**: *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 44*

Watahiniwa 771,624 (69.7%) walipata 0 katika swali hili. Watahiniwa hao walishindwa kuandika athari yoyote kutokana na kutokuwa na maarifa kuhusu athari za tabianchi katika kilimo. Badala yake waliandika kuharibu eneo husika. Walitakiwa kueleza ni kwa namna gani eneo hilo linaharibika kama kukata miti na ongezeko la joto duniani. Watahiniwa hawa walihusianisha mabadiliko ya tabia nchi na athari za mazingira zitokanazo na shughuli za binadamu.

Kielelezo Na. 8 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa.


SWALI LA 44


i) ukataji wa miti ovyo

ii) Kuchoma misitu

**Kielelezo Na. 8**: *Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 44*

**Swali la 45:** Mwanafunzi wa Darasa la Nne alichora ramani ambayo wenzake walishindwa kutambua ni ya eneo gani na lenye ukubwa upi? Je, ni vipengele vipi vya ramani ambavyo hakuvizingatia?


Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubainisha vipengele viwili vya ramani vinavyopaswa kuzingatiwa ili kutambua jina la eneo na ukubwa wa eneo husika kwa kutumia ramani. Kwa ujumla ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa ni wa wastani kwani watahiniwa 138,717 (12.5%) walipata alama zote 02, watahiniwa 417,134 (37.7%) walipata alama 01, na watahiniwa 551,948 (49.8%) walipata 0. Chati Na. 16 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 45.




**Chati Na. 16**: *Ufaulu mzuri wa watahiniwa katika swali la 45*


Watahiniwa 138,717 (12.5%) waliopata alama 02, waliweza kuandika majibu sahihi ambayo ni Kipimio cha Ramani au Skeli na Kichwa cha Ramani. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu vipengele vya ramani vinavyomwezesha msoma ramani kutambua eneo na ukubwa wa eneo halisi. Kichwa cha ramani hutambulisha ramani inahusu nini, wakati kipimio huonesha uhusiano ulipo kati ya umbali uliopo katika ramani na umbali halisi kwenye ardhi.

Vile vile, watahiniwa 417,134 (37.7%) walipata alama 01 kwa kuandika jibu moja sahihi na lingine lisilo sahihi, au waliandika jibu moja tu sahihi. Hii inatokana na kuwa na maarifa ya wastani kuhusu vipengele vya ramani, au kutokuelewa swali kwa ufasaha. Kielelezo Na. 9 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa.


SWALI LA 45
i) Kipimio Cha ramani
ii) Kichwa Cha ramani

**Kielelezo Na. 9**: *Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 44*

Hata hivyo, watahiniwa 551,948 (49.8%) walipata 0 katika swali hili. Watahiniwa hao walishindwa kwa kuwa hawakuwa na maarifa kuhusu mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa usomaji wa ramani. Badala yake, walitoa majibu yasiyo sahihi. Hii inaonyesha wanafunzi hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya vipengele muhimu katika ramani. Kielelezo Na. 10 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa.


SWALI LA 45
Ufunguo

**Kielelezo Na. 10**: *Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 45*

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA KILA UMAHIRI

Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa katika umahiri uliotahiniwa katika somo la Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi unaonesha kutofautiana kwa ufaulu kulingana na umahiri husika. Watahiniwa walibainishwa kuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kupata asilimia kuanzia 60-100, ambako kumeoneshwa kwa rangi ya kijani katika jedwali. Vilevile, watahiniwa walibainishwa kuwa wamefaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata kati ya asilimia 40-59. Ufaulu katika jedwali umeoneshwa kwa rangi ya njano. Kwa upande mwingine, ufaulu wa kiwango hafifu ulibainishwa kwa kupata kati ya asilimia 0-39. Kiwango cha ufaulu huu kimeoneshwa katika jedwali kwa rangi nyekundu.

Umahiri uliotahiniwa katika PSLE 2021 somo la Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi ni *Kutambua matukio yanayotokea katika mazingira yanayomzunguka, Kutambua misingi ya uzalendo katika jamii*, *Kutumia ramani na elimu ya anga katika maisha ya kila siku*, *Kufuata kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishaji mali*, *Kutumia misingi ya unadhifu*, *Kumudu mapishi mbalimbali*, *Kusanifu kazi za sanaa* na *Kutumia stadi za ujasiriamali*. Uchambuzi unaonesha kuwa, ufaulu katika umahiri wa *Kusanifu kazi za sanaa* (57.3%), *Kumudu mapishi mbalimbali* (55.9%), *Kutumia ramani na elimu ya anga katika maisha ya kila Siku* (53.8%), *kutambua misingi ya uzalendo katika jamii* (41.5%), *Kutumia misingi ya Unadhifu* (39.9%) na *Kutambua matukio yanayotokea katika mazingira yanayomzunguka* (39.9%) ulikuwa wa kiwango cha wastani.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, ufaulu katika umahiri wa *Kufuata kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishaji mali* (33.6%) na *Kutumia stadi za ujasiriamali* (25.1%) ulikuwa ni wa kiwango hafifu.

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani wa Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi umeonesha kuwa, watahiniwa 788,528

(71.21%) walifaulu kwa kupata kati ya daraja A-D. Hata hivyo kumekuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu kwa umahiri wa *kusanifu kazi za sanaa*, *kumudu mapishi mbalimbali*, *kutumia ramani na elimu ya anga katika maisha ya kila siku*, *kutambua misingi ya uzalendo katika jamii*, *kutumia misingi ya unadhifu* na *kutambua matukio yanayotokea katika mazingira yanayomzunguka*.

Kwa upande mwingine, kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika umahiri wa *kutafuta kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishaji mali* na *kutumia stadi za ujasiliamali* kilikuwa ni hafifu.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuboresha zaidi kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika somo la Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi, Baraza la Mitihani la Tanzania linapendekeza mambo yafuatayo:

(a) Ufundishaji na ujifunzanji wa umahiri uliobainika kuwa na ufaulu hafifu ambao ni *kutafuta kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishajimali* na *kutumia stadi za ujasiliamali* uzingatie mbinu mbalimbali za ufundishaji ikiwa ni pamoja na;

(i) Walimu kuandaa maigizo, na kuwashirikisha wanafunzi katika michezo mbalimbali kama njia ya ziada katika ufundishaji na ujifunzaji wa umahiri kama *kutambua misingi ya uzalendo katika jamii*, *kutumia misingi ya unadhifu* na *kutambua matukio yanayotokea katika mazingira yanayomzunguka*.

(ii) Walimu kutumia njia ya ziara za kimasomo ili kuwawezesha wanafunzi kujifunza katika mazingira halisi ili kuwapa hamasa ya kujifunza zaidi.

(iii) Walimu kutumia njia ya kazi mradi katika umahiri wa *kusanifu kazi za sanaa* na *kumudu mapishi mbalimbali* katika kukazia maarifa wanayojifunza wanafunzi.

(iv) Walimu kutumia michoro, ramani na picha mbalimbali kufafanua dhana tofauti wakati wa ufundishaji na ujifunzaji.

(b) Wanafunzi washauriwe na kusisitiziwa kusoma kwa bidii vitabu vya kiada na ziada ili kuongeza maarifa na ujuzi ambao utawawezesha kujibu maswali ya mtihani kwa usahihi.

(c) Mamlaka husika zifanye utafiti wa kubaini changamoto zinazozuia ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji, na kuziondoa ili kuongeza kiwango cha ufaulu.

(d) Walimu wapewe mafunzo ili ufundishaji na ujifunzaji uzingatie uwepo wa maboresho yaliyofanyika katika mtaala. Pia, namna ya kutunga maswali yatakayozingatia umahiri ili kuwajengea wanafunzi uzoefu unaostahili katika kujibu maswali katika mitihani.

**Kiambatisho**

## MUHTASARI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA SOMO LA MAARIFA YA JAMII NA STADI ZA KAZI

| Na. | Mada | Na. ya Swali | Ufaulu katika kila Swali (%) | Wastani wa Ufaulu katika kila Umahiri (%) | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Kusanifu kazi za sanaa | 36 | 57.3 | 54.9 | Wastani |
| 2. | Kumudu mapishi mbalimbali | 38 | 55.9 | 53.8 | Wastani |
| 3. | Kutumia ramani na elimu ya anga katika maisha ya kila siku | 24 | 74.3 | 53.8 | Wastani |
| | | 25 | 47.7 | | |
| | | 26 | 52.0 | | |
| | | 27 | 57.8 | | |
| | | 28 | 40.5 | | |
| | | 45 | 50.2 | | |
| 4. | Kutambua misingi ya uzalendo katika jamii | 12 | 87.1 | 41.5 | Wastani |
| | | 13 | 44.9 | | |
| | | 14 | 25.5 | | |
| | | 15 | 41.0 | | |
| | | 16 | 73.0 | | |
| | | 17 | 76.5 | | |
| | | 18 | 23.4 | | |
| | | 19 | 56.0 | | |
| | | 20 | 15.2 | | |
| | | 21 | 34.6 | | |
| | | 22 | 24.6 | | |
| | | 23 | 25.8 | | |

| Na. | Mada | Na. ya Swali | Ufaulu katika kila Swali (%) | Wastani wa Ufaulu katika kila Umahiri (%) | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 42 | 11.5 | | |
| 5. | Kutumia misingi ya unadhifu | 39 | 63.3 | 39.9 | Wastani |
| | | 40 | 16.5 | | |
| 6. | Kutambua matukio yanayotokea katika mazingira yanayomzunguka | 1 | 10.0 | 39.9 | Wastani |
| | | 2 | 65.9 | | |
| | | 3 | 30.4 | | |
| | | 5 | 25.4 | | |
| | | 7 | 46.3 | | |
| | | 8 | 47.6 | | |
| | | 9 | 45.5 | | |
| | | 10 | 50.8 | | |
| | | 11 | 44.2 | | |
| | | 41 | 43.8 | | |
| | | 43 | 15.6 | | |
| 7. | Kufuata kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishaji mali | 4 | 50.0 | 33.6 | Hafifu |
| | | 6 | 40.2 | | |
| | | 29 | 35.7 | | |
| | | 30 | 32.7 | | |
| | | 31 | 22 | | |
| | | 32 | 28.9 | | |
| | | 33 | 59.2 | | |
| | | 34 | 19.9 | | |
| | | 35 | 17.4 | | |
| | | 44 | 30.2 | | |
| 8. | Kutumia stadi za ujasiriamali | 37 | 25.1 | 25.1 | Hafifu |